# Nipashe

Ijumaa Mei 7, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580573

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAM

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




**Mlinzi** amuua mke kikatili na yeye kujiua kwa sumu

UKURASA 2



**Rais** Samia kuteta na wazee 900 wa Dar es Salaam leo

UKURASA 2

**Mbappe akaribia kusaini Real Madrid**

UKURASA 20



# Sukari, mafuta ya kula havikamatiki

UKURASA 4


## YALIYOMO

UKURASA WA 3

**POLISI DAR YAFUNGUKA KUHUSU KUSHAMIRI WIZI**

WAKATI operesheni maalum dhidi ya wezi wa vifaa vya magari, pikipiki na uvunjaji...

UKURASA WA 5

**SABABU ZA VIFO KIPINDI CHA MFUNGO ZATAJWA**

MKURUGENZI Mtendaji wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), Prof. Mohamed...


## Miradi 1,500 kumaliza ukosefu wa maji nchini

UKURASA 3



Wafanyabiashara maarufu nchini, James Rugemalira na Harbinder Seth Singh, wakiwa chini ya ulinzi wa askari Magereza, baada ya kesi inayowakabili ya uhujumu uchumi kutajwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana. Wafanyabiashara hao wana takribani miaka minne mahabusu tangu kesi yao ilipotajwa kwa mara ya kwanza mahakamani hapo Juni, 2017. **PICHA: JUMANNE JUMA**





Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play

App Store

# Madaktari wazungumzia kirusi kipya cha corona

UKURASA 2


**MICHEZO** **SIMBA, YANGA HAKUNA MNYONGE** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Adaiwa kumuua mke kisha naye kujiua

**Na Tumaini Mafie,** ARUMERU

MLINZI wa Kampuni ya Ulinzi ya Intelligence ya Arusha, Elias Mollel (34), amemuua kikatili mwenzi wake, Neema Gasper, kwa kumchinja shingo kisha kujiua kwa kutumia sumu ya panya.

Mollel, mkazi wa Olmotony katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Ngaramtoni, wilayani Arumeru, kabla ya kukatisha uhai wake na mpenzi wake, anadaiwa kuandika waraka maalum wazikwe kaburi moja na mke wake na wasitenganishwe.

Jana, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Kamishna Msaidizi (ACP) Justine Masejo, alithibitisha tukio hilo kuwa lilitokea juzi.

"Uchunguzi wetu wa awali unaonyesha kwamba huyu Mollel alimuua mpenzi wake Neema mwenye umri wa miaka 21. Hawa walikuwa wanaishi nyumba moja waliyopanga huko Olmotony, Ngaramtoni.

"Kinachoonekana ni wivu wa mapenzi. Huyu Mollel alimkata mpenzi wake kwa kitu chenye ncha kali shingoni na kisha yeye kunywa sumu ya panya iliyosababisha umauti wake," alisema Kamanda Masejo.

Alisema miili ya wapenzi hao imehifadhiwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Arusha ya Mount Meru, ikisubiri uchunguzi zaidi wa kitabibu.

Akizungumzia tukio hilo, mmoja wa viongozi wa Kitongoji cha Olmotony, Lucas Kesoi, alisema katika chumba walichokuwa wamelala wapenzi hao, waliwakuta wamelala pamoja kitandani, huku damu zikiwa zimetapakaa chini.

"Baada ya kufika katika nyumba waliyokuwa wanakaa, nilifungua mlango nikakuta miili miwili, mmoja wa mume (Mollel) ulikuwa unaning'inia kitandani na mwili wa mwanamke (Neema) ulikuwa umefunikwa ukiwa kitandani.

"Nilishindwa cha kufanya, ikabidi nitafute msaada wa polisi ili waje wafanye ukaguzi na kuiondoa miili hiyo kwenda kuihifadhi hospitalini. Neema alikuwa amepanga katika nyumba hiyo muda mrefu na ndiye aliyemkaribisha huyu Mollel," alisema.

### AACHA UJUMBE MZITO

Kwa mujibu wa Kesoi, Mollel aliacha ujumbe wa maandishi, akiomba msamaha kwa uamuzi aliochukua wa kumuua mpenzi wake kisha na yeye kujiua.

Kesoi alieleza kuwa sehemu ya ujumbe huo uliokuwa kwenye karatasi unaeleza hivi: "Wazazi wangu, nisameheni kwa kuchukua uamuzi niliofanya, ila naomba nizikwe na mke wangu kaburi moja."

Jirani aliyekuwa amepanga vyumba karibu na marehemu hao, Rodrick Lymo, alisema aliuona mlango wa chumba chao ukiwa wazi muda mrefu na sauti ya redio ikiwa juu.

# Madaktari wazungumzia kirusi kipya cha corona

**Na Elizabeth Zaya**

RAIS wa Chama cha Madaktari Tanzania (MAT), Dk. Shadrack Mwaibambe, ameeleza namna kirusi kinavyoweza kubadilika kwa kuwa na makali zaidi au kudhoofu.

Akizungumza na Nipashe alipoulizwa endapo kuna ukweli wowote kuhusu kuwapo kwa kirusi kipya cha ugonjwa wa corona katika baadhi ya nchi, Dk. Mwaibambe alisema mpaka sasa hawajathibitisha endapo kuna uwapo wa kirusi kipya katika nchi hizo zinazotajwa watu wake kufariki kwa wingi kwa ugonjwa huo.

"Ni kweli tunasikia kwamba kuna ujio wa kirusi kipya cha corona katika baadhi ya nchi hasa zile ambazo kwa sasa zinaonekana kupoteza watu wake kwa wingi, lakini mpaka sasa hakuna utafiti kwamba hicho kinachoua huko ni kipya au laa," alisema Dk. Mwaibambe.

"Lakini niseme kwamba kama ni kirusi kipya kweli, huwa hakina mipaka, kwa sababu nchi yetu siyo kisiwa, hata kwetu kinaweza kuingia wakati wowote. Kinachotakiwa ni kuchukua tahadhari za kujikinga kama tulivyokuwa tunachukua awali na kuepuka hofu kwa sababu hiyo nayo huchangia kuleta athari zaidi."

Dk. Mwaibambe alisema ili wananchi kuwa salama zaidi ni vema kuendelea kuchukua tahadhari kwa sababu kirusi kinapobadilika mara kadhaa huwa kina matokeo tofauti aidha, kinakuwa na makali zaidi ya yale ya awali au makali yake kudhoofika.

"Maisha ya kirusi mara zote huwa kinabadilika na hii ni hata kabla ya ujio wa hiki cha corona, huwa kinabadilika. Na kinapobadilika mara tatu au mara tano huwa wakati mwingine kinakuwa na makali zaidi au makali yake yanadhoofika," alisema Dk. Mwaibambe.

"Na kinapobadilika mara tatu au mara tano kwa makali kinaweza kuleta madhara zaidi, kinaweza kukwepa hata kinga ya mwili, kina uwezo wa kuathiri mtu yeyote aliye na kinga nyingi au asiye na nyingi."

"Kinachotakiwa kufanywa ni kuchukua tahadhari. Na katika hili kitaalamu huwa hatushauri watu kuwa na hofu, kwa sababu hofu ikiathiri afya ya akili inakuwa na hatari zaidi na watu wanaweza kupoteza maisha kwa sababu hiyo."

Alisema kinachohitajika kunapotokea uwapo wa mabadiliko ya kirusi kinacholeta athari kwa wananchi hususani hicho cha ugonjwa wa corona, ni kutumia utashi kuwaandaa wananchi namna ya kuchukua tahadhari ya kukabiliana nacho bila kuleta hofu.

"Na ndiyo maana tunashauri kwamba zile tahadhari zilizokuwa zikichukuliwa kwa kutumia mwongozo wa Wizara ya Afya zifuatwe, watu wavae barakoa kwa sababu inasaidia...narudia inasaidia na kuchukua tahadhari zote zinazoshauriwa kitaalamu," alisisitiza Dk. Mwaibambe.

"Tahadhari zote zichukuliwa na kuepuka mikusanyiko isiyo ya lazima wakati wakiendelea na shughuli zao za kila siku."

"Tunapongeza hatua ambazo pia serikali imekuwa ikizichukua kupambana na ugonjwa huu wa corona na pia ambazo imeanza kuzichukua sasa ikiwamo kusitisha baadhi ya safari kutoka kwenye baadhi ya nchi.

Tunaamini utashi wa kisiasa utaendelea kuchukuliwa katika kuelimisha wananchi juu ya hili bila kuleta hofu kama ambavyo serikali imekuwa ikifanya."

Aprili 6, mwaka huu, akiapisha Makatibu Wakuu, Manaibu Makatibu Wakuu na Wakuu wa Taasisi na Idara za serikali, Rais Samia Suluhu Hassan alisema anakusudia kuunda jopo la wataalamu kwa ajili ya kuangalia suala la ugonjwa huo wa corona kwa upana zaidi na liishauri serikali hatua za kuchukua kwa sababu Tanzania siyo kisiwa.

"Ninakusudia kuunda kamati ya wataalamu waliangalie suala la corona kwa upana wake na kitaalam halafu watushauri serikali."

"Halifai kulinyamazia, kulikataa au kulikubali bila kufanya utafiti wa kitaalamu, tutafanya utafiti wa kitaalamu, tutaunda wataalamu, watuambie upeo wa swali au tatizo hili lilivyo na hayo yanayopendekezwa na ulimwengu kuja kwetu, je, yakoje kitaalamu, kwa utaalamu wetu wa ndani."

India ni miongoni mwa nchi ambazo zimekumbwa na wimbi la pili la kirusi cha corona na juzi Shirika la Afya Duniani (WHO) lilisema nchi hiyo kwa wiki moja iliyopita ilirekodi asilimia 46 ya watu waliofariki kwa ugonjwa huo nchini humo.



Rais Samia Suluhu Hassan, akiongoza kikao cha Baraza la Mawaziri, Ikulu Chamwino, jijini Dodoma jana. **PICHA: OMR**

# Rais Samia kuteta na wazee wa Dar es Salaam

**Na Idrisa Sadick**

RAIS Samia Suluhu Hassan leo anatarajia kuzungumza na wawakilishi 900 wa wazee wa mkoa wa Dar es Salaam kwa lengo la kujadili mambo mbalimbali yanayowahusu wazee.

Mkuu wa Mkoa huo, Aboubakar Kunenge, alisema hayo jana katika taarifa yake huku akibainisha kwamba mkutano huo utafanyika katika ukumbi wa mikutano wa Mlimani City kuanzia saa 8:00 mchana.

Alisema idadi hiyo ya wazee waliopatiwa mwaliko pekee ndio wanaotarajiwa kuhudhuria katika kikao hicho huku akiwasihi wazee hao kutii wito wa Rais ili kuhakikisha lengo la mkutano linatimia.

"Wale tu ambao wamepata mialiko ndio tunatarajia watahudhuria mkutano huo. Wazee wengine ambao hawakupata mialiko pamoja na wakazi wengine wa mkoa wa Dar es Salaam na Watanzania wote kwa ujumla tunawaomba sana kufuatilia mkutano huo kupitia vyombo vya habari," alisema.

Alisema baadhi ya wazee waliopokea wito huo, wameahidi kujitokeza ili kupata nafasi ya kumweleza Rais Samia matatizo yao.

# Miradi 1,500 kumaliza tatizo la maji

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

TATIZO la upatikanaji wa majisafi na salama nchini linatarajiwa kupatiwa ufumbuzi baada ya serikali kupanga kutekeleza miradi 1,527 katika maeneo ya vijijini na miradi 114 maeneo ya mijini ikihusisha miradi mipya, upanuzi na ukarabati wa miundombinu.

Serikali pia imepanga kuchimba visima 516, kujenga mabwawa 33 hususani katika maeneo yenye ukame nchini.

Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, alitangaza neema hiyo jana bungeni wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara yake kwa mwaka wa fedha 2021/22, huku akiomba Bunge kuidhinisha Sh. bilioni 680.388.

Pia alisema serikali imepanga kuimarisha taasisi zinazosimamia utoaji wa huduma za maji na usafi wa mazingira nchini, vikiwamo vyombo vya watumia maji (CBWSO), mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira, Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini na kusimamia ufuatilia wa utekelezaji wa miradi.

Kuhusu Mkoa wa Dar es Salaam na baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Pwani, Waziri Aweso alisema serikali inaendelea na miradi ya ukarabati na upanuzi wa mfumo wa usambazaji maji safi unaogharimu Sh. bilioni 200.818 kwa fedha kutoka Benki ya Dunia.

Alisema kati ya fedha hizo, Sh. bilioni 130.765 ni kwa ajili ya ujenzi wa matangi na kupanua mtandao wa kusambaza maji wenye urefu wa kilomita 1,440 na kuunganisha wateja wapya 64,000 na kwamba mkandarasi ameajiriwa na yuko katika eneo la mradi.

Waziri Aweso pia alisema Dola za Marekani milioni 20 (Sh. bilioni 46.376) ni kwa ajili ya kutekeleza mradi wa kupunguza upotevu wa maji ambao uko kwenye hatua za kupata wataalamu washauri wa kusimamia mradi.

Alisema Dola za Marekani milioni 10 (Sh. bilioni 23.188) ni kwa ajili ya ununuzi wa dira za maji 50,000 na taratibu za kumpata mzabuni zinaendelea.

Waziri Aweso alisema: "Hadi Machi, mwakani, mradi wa maji kutoka matangi ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) hadi Bagamoyo umefikia asilimia 22. Mradi huo unatarajiwa kutekelezwa kwa miezi 36 na kukamilika Desemba 2022."

Alisema wizara inatekeleza miradi ya kuboresha huduma ya majisafi na usafi wa mazingira katika mkoa wa Dar es Salaam pamoja na maeneo ya Kibaha, Kisarawe, Mkuranga, Chalinze na Bagamoyo.

Waziri Aweso aliitaja miradi hiyo kuwa ni ya visima virefu vya Kimbiji na Mpera na kwamba kwa upande wa Kimbiji ni visima 12 na Mpera visima vinane. Gharama za mradi huo ni Sh. bilioni 18 na vinatarajiwa kuzalisha maji lita milioni 260 kwa siku.

Alisema hadi kufikia Machi, mwaka huu, uchimbaji wa visima 14 umekamilika na kati ya hivyo, 11 ni vya Kimbiji na vitatu ni vya Mpera. Alisema visima vinne vya Kimbiji na kimoja cha Mpera vimekamilika kwa kiwango cha kufaa kuwekewa miundombinu ya kusambaza maji.

Waziri Aweso alibainisha kuwa ukamilishaji wa visima vilivyobaki unaendelea na unatarajiwa kukamilika Desemba, 2021.

"Kwa upande wa usambazaji wa maji, ujenzi wa miradi umeanza kutoka katika visima vya Kimbiji ambapo utekelezaji wake umegawanywa katika vipande vinne. Kipande cha kwanza kinahusu ujenzi wa miundombinu ya kutoa maji kwenye visima kwenda kwenye pampu kubwa ambapo mkandarasi yupo katika hatua ya mwanzo," alisema.

Aliongeza: "kipande cha pili kinahusu ujenzi wa kituo cha kusukuma maji pamoja na bomba la kutoa maji kwenda kwenye tangi la kuhifadhia lenye ujazo wa lita milioni 15 eneo la Kisarawe II, ambapo utekelezaji umefikia asilimia 35, na maandalizi ya utekelezaji wa kipande cha tatu na nne vinavyohusu miundombinu ya usambazaji maji yanaendelea."

Waziri Aweso alisema serikali kwa kushirikiana na Serikali ya India inaendelea kutekeleza awamu ya tatu ya Mradi wa Maji Chalinze kwa gharama ya Sh. bilioni 41.3. Alisema mradi huo umelenga kunufaisha vijiji 68 ambapo vijiji 19 viko kaskazini na 49 viko kusini mwa mto Wami.

Alibainisha kuwa hadi kufikia Machi 2021, utekelezaji wa mradi huo umefikia wastani wa asilimia 87.5 na unatarajiwa kukamilika Oktoba, mwaka huu.

# Sababu kushamiri wizi Dar zatajwa

**Na Romana Mallya**

WAKATI operesheni maalum dhidi ya wezi wa vifaa vya magari, pikipiki na uvunjaji ikiendelea kufanywa na Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, imeelezwa kuwa baadhi ya wafungwa waliotoka gerezani, wakiwamo waliosamehewa, wanaendelea na vitendo vya wizi na uhalifu.

Kamanda wa Kanda hiyo, Lazaro Mambosasa, alithibitisha hilo alipozungumza na Nipashe kwa njia ya simu jana.

Alisema katika operesheni ya siku saba iliyofanyika kuanzia Aprili 26, mwaka huu, wamewakamata watuhumiwa 161 huku Aprili 24, idadi ilikuwa watu 49 ambao bado hawajafikishwa mahakamani.

Mambosasa alisema watu hao waliopata msamaha wa Rais, baada ya kutoka kwenye magereza, wanaungana na wenzao wa nje kuendesha uhalifu huo.

Kuhusu vitendo vya wizi kwenye makazi ya watu ambapo baadhi ya maeneo watu wanalalamika kutokea, Kamanda Mambosasa alisema kupitia operesheni inayoendelea wanakamata vibaka na wezi wakubwa.

Akiwazungumzia watuhumiwa 161 waliokamatwa katika operesheni hiyo endelevu, alisema wametokana na wenzao 49 ambao walikamatwa awali na kukiri na kutaja wanaoshirikiana nao katika wizi wa vifaa vya magari, pikipiki na uvunjaji.

Alisema vinara hao wa wizi wa pikipiki wamekamatwa Zanzibar wakiwa na pikipiki 40 za wizi ambazo wamekuwa wakiziiba Dar es Salaam, Morogoro na Pwani na kuzipeleka visiwani humo kutafuta wateja.

Mambosasa alisema katika operesheni hiyo wamekamata magari mawili aina ya Toyota



Noah namba T 770 ACY na Toyota IST lenye namba T 137 DMM, ambayo yaliibwa mwezi uliopita.

BABU MBARONI

Kamanda Mambosasa alisema wanamshikilia Said Abdallah (61) kwa tuhuma za wizi kwenye maghala na maduka kwa kutumia funguo bandia 83 alizokutwa nazo pamoja na misumari ya aina mbalimbali 47 ambayo ni malighafi za kutengenezea funguo hizo.

Mambosasa alisema mtuhumiwa huyo baada ya kuhojiwa amekiri kufanya uhalifu tangu mwaka 2013 maeneo mbalimbali ya Dar es Salaam.


**International School of Tanganyika**
Challenge | Support | Inspire

## Invitation For Bids

Bids are invited from interested registered, competent, reliable and licensed suppliers/dealers to provide the under listed goods and services for the year ending 31st July 2022.

| S/N | Category No. | Description |
|---|---|---|
| 1. | Category 1 | Maintenance Materials |
| 2. | Category 2 | Consumables and Cleaning Materials |
| 3. | Category 3 | Office Stationery |
| 4. | Category 4 | Staff Welfare Supplies (Sugar, Tea, Coffee & Milk Powder) |
| 5. | Category 5 | Timber |
| 6. | Category 6 | Servicing of Fire Extinguishers |
| 7. | Category 7 | Fumigation |
| 8. | Category 8 | Cesspit Emptying |
| 9. | Category 9 | Appliances (Fridges, Cookers & Air-conditions) |
| 10. | Category 10 | Motor Vehicle Spare Parts |

**Conditions:**

- Bid document(s) will be emailed to the bidders on payment of **TZS. 50,000/=** payable per bid category. Payments should be made to the Billing Department located in the Administration Building (Gate #5), off United Nations Road, Upanga, between 10.00 am to 1.00 pm Monday to Friday. Bidders will need to provide the School with the **email ID** at the time of making payment. Once payment has been received, bid documents will be emailed by the following working day.
- Bids should be emailed to bids@istafrica.com latest by **2 p.m. on Friday, May 21, 2021.** No bids will be accepted after this time. In addition, bidders should attach scanned copies of certificates of registration, business license, TIN/VAT certificates and User Identification Number certificate (for VAT registered suppliers). On submission of the information, the bidders would receive a confirmation that their bids have been successfully received by IST.
- The School is not bound to accept the lowest or any bid and reserves the right to reject all or any of the bids received.

# Sukari, mafuta ya kula havikamatiki

**Na Waandishi Wetu**

BEI za mafuta ya kula na sukari zimezidi kupaa huku bidhaa moja ikiadimika nchini, kiasi cha wananchi kuhangaika kuipata na wengine kushindwa kumudu bei iliyopo sokoni.

Mafuta ya kula yalianza kuadimika nchini Juni, mwaka jana, na serikali ilieleza kuwa chanzo ni janga la corona lililosababisha shehena iliyoagizwa nje kujazia upungufu unaokuwapo nchini kushindwa kuwasili kwa wakati.

Aprili, mwaka huu, Waziri wa Viwanda na Biashara, Prof. Kitila Mkumbo, katika mahojiano maalum na gazeti hili, alisema meli mbili zenye shehena ya mafuta ya kula zimewasili nchini na nyingine ingefika Aprili 29, mwaka huu, ili kupunguza makali ya bidhaa hiyo.

Pia alisema kuhusu sukari serikali imeweka bei elekezi ya Sh. 2,600 kwa kilo, huku ikiwatahadharisha wafanyabiashara kutotumia uwapo wa mfungo wa mwezi wa Ramadhani kupandisha bei ya bidhaa hiyo.

Desemba 10, mwaka huu serikali ilieleza kupokea shehena ya tani 21,800, Januari 16, mwaka huu, tani 26,500 za mafuta yaliyoagizwa na kampuni na viwanda mbalimbali katika kukabili uhaba wa bidhaa hiyo, na kwamba Februari ingeingia shehena nyingine.

Aliyekuwa Waziri wa Viwanda na Biashara, Geoffrey Mwambe, alisema mafuta nchini kwa mwezi ni tani 'metrick' 30,000 ya nje, tofauti na yanayozalishwa ndani ya karanga na alizeti.

Tofauti na maelezo ya serikali, bidhaa hizo zimezidi kupaa na katika maeneo mengi nchini na kilo moja ya sukari imefikia Sh. 2,800 hadi 3,000 na mafuta yamfikia Sh. 36,000 kwa lita tano.

Nipashe ilifuatilia katika maeneo mengi nchini na kubaini kuwa bei ya mafuta inazidi kupaa, huku bidhaa hiyo ikikosekana sokoni na bei ya kipimo kidogo ikipanda kutoka Sh. 500 hadi 1,000 na maeneo mengine Sh. 1,500.



Waziri wa Viwanda na Biashara, Prof. Kitila Mkumbo

**DAR MSHIKEMSHIKE**

Mkoani Dar es Salaam, mafuta ya alizeti lita moja hayapatikani huku mafuta ya lita tatu yanapatikana kwa bei ya Sh. 22,000 hadi 25,000 kutoka Sh. 15,000 hadi 17,000. Lita tano ya mafuta ya alizeti imefikia Sh. 36,000 katika maeneo mengi Dar es Salaam na sababu kubwa ikidaiwa ni kuadimika kwa bidhaa hiyo nchini.

Eneo la Mwenge, mathalan, lita tano yanauzwa kati ya Sh. 37,000 hadi Sh. 39,000 na yale ya lita tatu yanauzwa kati ya Sh. 25,000 na Sh. 28,000.

Kwa upande wa sukari, kilo moja inauzwa kati ya Sh. 2,700 na Sh. 3,000 kulingana na eneo.

Tabata jijini Dar es Salaam mafuta ya alizeti wanauza lita tano Sh. 35,000, lita tatu Sh. 25,000 na lita moja Sh. 15,000. Mafuta aina isiyotokana mimea aina ya Korie Lita tano yauzwa Sh. 27,000, lita tatu Sh. 17,000 na lita moja Sh. 6000.

**DODOMA**

Kilo moja ya sukari inauzwa Sh. 2,800 hadi 3,000, huku maduka ya jumla yakiuza mfuko wa kilo 25 Sh. 62,500.

Mafuta hususani ya alizeti, lita tano yanauzwa kati ya Sh. 20,000 hadi 22,000 wakati yale ambayo yamechujwa mara mbili ambayo watu hupikia bila kuchemshwa yanauzwa Sh. 17,000 kwa lita tatu huku lita tano ikiuzwa Sh. 29,000 hadi Sh. 30,000.

Mafuta ya Sundrop katika jiji hilo yanauzwa kwa lita tano Sh. 38,000 katika maduka ya kawaida na maduka makubwa (Supermarket) Sh. 41,000 kwa lita tano huku lita tatu yakiuzwa kwa Sh. 20,000 maduka ya kawaida na 'supermarket' Sh. 21,000.

**ARUSHA**

Kaimu Meneja wa Kampuni ya Mohamed Enterprises ya Arusha, Ally Manji, alisema jana hali ya upatikanaji wa sukari kwa mkoa huo ni mgumu kutokana na viwanda vya ndani kusitisha uzalishaji kwa ajili ya kufanya matengenezo ya mitambo.

"Nchi jirani sukari inauzwa kwa bei ya juu kidogo, tofauti na ya nchi yetu. Sisi tunauza Sh. 120,000 kwa mfuko wa kilo 50, lakini sukari ya Uganda inauzwa kwa Sh. 122,000 kwa ujazo huo huo," alisema.

Kwa upande wa mafuta katika baadhi ya maduka, yanauzwa kwa ndoo ya lita 10 Sh.45,000, lita 20 kwa Sh.89,000 hadi 91,000, lita tano Sh. 25,000 na lita tatu ikiwa Sh. 16,000.

Mafuta ya Sunbelt lita 10 inauzwa kwa Sh. 62,000, lita tano Sh. 32,000 na lita 20 Sh. 125,000, huku mafuta ya Sundrop lita 10 yakiuzwa kwa Sh. 60,000, lita tano Sh. 30,000 na lita tatu Sh. 20,000. Mafuta ya Fresh Free lita tano yanauzwa kwa Sh. 25,000.

**MOSHI**

Katika mji wa Moshi, bei za mafuta ya kula zimepanda kutoka Sh. 2,500 hadi 7,600 kwa ujazo wa lita moja na sukari kilogramu moja, imepanda kutoka Sh. 2,200 hadi Sh. 2,900.

Mmoja wa wafanyabiashara wa mafuta ya chakula, Anastasia Jones, alisema mafuta hayo yamepanda, akitolea mfano mafuta ya alizeti ya ujazo wa lita moja yamepanda kutoka Sh. 2,500 hadi 6,000 kwa lita moja, lita tano yanauzwa kwa Sh. 36,000 na lita 20 yanauzwa kwa Sh. 11 8,000.

Katika mji wa Kibaha mkoani Pwani, lita moja ya mafuta inauzwa kati ya 4,400 hadi 4,500 huku sukari kilo moja ikiuzwa kwa Sh. 3,000 kutoka 2800 bei ya awali.

**IRINGA**

Lita tano ya mafuta aina ya Sundrop yanauzwa Sh. 40,000 wakati mafuta aina ya Golden ni Sh. 37,000 na lita tatu ya mafuta ya Golden ni Sh. 23,000 na Sundrop ni 26,000. Kwa upande wa sukari, kilo moja ni Sh. 2,800 hadi Sh. 2,900 na upatikanaji wake ni wa kawaida.

Mjini Morogoro, mfanyabiashara katika stendi ya Msamvu, Mariam Mbena, alisema kwa sasa wanalazimika kununua sukari kwa kilo moja Sh. 2,800 wakati inapaswa kuuzwa 2,200 mpaka 2,400 kwa bei ya rejareja katika maduka mbalimbali.

Aidha, mafuta ya kula yanauzwa lita moja Sh. 3,800 mpaka 4,000 kwa mafuta aina ya Korie.

**KANDA YA ZIWA**

Katika Jiji la Mwanza, kilo moja ya sukari katika maduka mengi imepanda kutoka Sh. 2,600 hadi 2,800 huku mafuta ya kula lita moja aina ya Korie yakiuzwa Sh. 5,500 kutoka Sh. 5,000.

Mjini Musoma, mkoani Mara, lita tano za mafuta yanauzwa Sh. 27,000 kutoka Sh. 25,000 kwa mwezi uliopita, huku sukari nayo ikiuzwa kati ya Sh. 2,700 hadi Sh. 2,800 kutoka Sh. 2,600 kwa kilo moja.

Manispaa ya Shinyanga, ndoo kubwa ya mafuta ya kula inauzwa Sh. 85,000 tofauti na Sh. 54,000 ya awali huku mfuko wa sukari kilo 50 ukiuzwa Sh. 133,000, kutoka Sh. 105,000.

Mfanyabiashara wa duka la rejareja Veronica Majida, alisema wananunua mafuta ya kula kwa Sh. 85,000 kwa ndoo kubwa, hivyo kuwalazimu kuuza mafuta lita moja Sh. 2,000 badala ya Sh. 1,200.

Pia alisema sukari wananunua mfuko wa kilo 50 Sh. 133,000 na kusababisha kuuza kilo moja kwa Sh. 2,800 kutoka 2,400.

**MTWARA MOTO**

Mkoani Mtwara katika Manispaa ya Mtwara/Mikindani, mafuta ya alizeti lita moja yanauzwa kwa Sh. 8,500 wakati awali ilikuwa kati ya Sh. 6,500 na 7,000. Lita tano ya mafuta hayo ni Sh. 37,000.

Mafuta aina ya Korie na Mo, kwenye maduka hayo yanauzwa lita moja kwa Sh. 5,000 kutoka bei ya awali ya Sh. 4,000 hadi 4,500 huku ndoo ya lita 10 ikiuzwa kwa Sh.45,000.

Aidha, kilo moja ya sukari inauzwa Sh. 2,700 na katika maduka mengine bei yake ni Sh. 2,800.



Mkuu wa Wilaya ya Kilolo, Asia Abdallah (kushoto), akifanya ukaguzi wa bidhaa mbalimbali katika maduka ya mjini Ilula, mkoani Iringa jana, ikiwamo bei ya sukari na mafuta ambayo imepanda zaidi. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

## HABARI KITAIFA



Mwenyekiti wa Bodi ya Chama cha Wanawake Wafanyabiashara Tanzania (TWCC), Mercy Sila, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu kumpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuteuliwa kuwa Rais wa kwanza mwanamke. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# CTI yahimiza uzalishaji bidhaa bora

**Na Romana Mallya**

MKURUGENZI Mtendaji wa Shirikisho la Wenye Viwanda Tanzania (CTI), Leodegar Tenga, amevitaka viwanda kuzalisha bidhaa zenye ubora wa kitaifa na kimataifa ili kuleta ushindani kwenye soko.

Tenga aliyasema hayo jana Dar es Salaam wakati akizindua kampeni ya 'Cover Max Ukiweka Umeweka' iliyoanzishwa na kiwanda cha uzalishaji wa mabati cha ALAF ambacho kimeleta bidhaa mpya ya mabati yenye rangi mbalimbali.

Alisema ili viwanda vya ndani vishindane ndani na nje ya nchi, ni lazima vizalishe bidhaa zenye ubunifu na ubora unaokidhi viwango vya kitaifa na kimataifa.

"Ninapongeza kiwanda cha ALAF ambacho ni wanachama wa CTI kwa kuwa wabunifu na wametengeneza bidhaa zenye ubora kwa kipindi cha miaka 60 tangu kuanzishwa kwake. Leo (jana) wamekuja na mabati yenye ubora ya rangi," alisema.

Tenga alisema Rais Samia Suluhu Hassan ndani ya kipindi kifupi tangu aapishwe, mara kwa mara amekuwa akizungumzia uboreshaji wa mazingira ya biashara ili kuvutia uwekezaji wa ndani na nje ya nchi.

"Hivyo wakati mazingira yanaendelea kuboreshwa ni lazima viwanda vilivyopo vihakikishe uchumi wa nchi unaendelea kukua kwa kutengeneza bidhaa bora zenye ushindani.

Ninawapongeza ALAF kwa juhudi mnazoziendeleza," alisema.

Meneja Mkuu wa kiwanda hicho, Paul Ray, aliihakikishia serikali kuwa bidhaa zinazozalishwa kiwandani hapo zina ubora na sasa wamezindua mabati hayo ya rangi yanayoendana na soko.

# Prof. Janabi ataja sababu za vifo kipindi cha mfungo

**Na Romana Mallya**

MKURUGENZI Mtendaji wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), Prof. Mohamed Janabi, amesema kumekuwa na ongezeko la matukio ya watu kupata mshtuko wa moyo kipindi cha mfungo na kusababisha vifo kutokana na ulaji wa chakula kingi kupita kiasi.

Katika mahojiano yaliyofanyika juzi, Prof. Janab alisema ulaji huo wa chakula kingi husababisha mabadiliko ya ghafla ya mzunguko wa damu kutoka kwenye moyo kwenda kusaidia umeng'enyaji tumboni.

Alisema wakati wa mfungo kwa wale wenye matatizo ya moyo na shinikizo la damu kuwa juu, ulaji wa chakula kingi kwa wakati mmoja kinaweza kuchochea mshtuko wa ghafla wa moyo.

Alisema mshtuko wa moyo husababisha vifo kwa milioni ya watu duniani na huwa vinaongezeka zaidi katika kipindi cha mfungo, sikukuu kubwa kama Pasaka, Iddi na Krismasi. "Kila mwaka huwa tunaona utafiti unaonyesha kwamba mshtuko wa moyo unaongezeka katika vipindi hivi. Nizungumzie Ramadhani ambayo kwa sasa inaendelea, kwa nini mshtuko wa moyo na kusababisha vifo, utafiti unaonyesha hutokea mara nne zaidi kuliko nyakati za kawaida," alisema.

Alitaja baadhi ya sababu kuwa mtu anapokula chakula kingi kwa wakati mmoja au kuvimbiwa tumbo hupanuka hivyo mwili huchukua damu iliyokuwa kwenye moyo na kupeleka kwenye njia ya chakula ili kusaidia umeng'enyaji.

"Huu mbadiliko wa ghafla wa damu unaweza kuwa kichocheo cha mshtuko wa moyo hasa kwa watu wenye matatizo ya moyo, pili, tumbo linapopanuka kwa sababu ya chakula kuwa kingi husababisha moyo kwenda haraka zaidi au unakwenda kawaida, lakini mapigo yanakuwa hayapo sawa sawa, hivi vyote vinachochea mshtuko," alisema.

Prof. Janab alisema magonjwa ya moyo yanaongoza vifo duniani na zaidi ya watu milioni 18 hufariki kila mwaka kwa sababu ya moyo hii ni asilimia 31 ya vifo vyote vinavyotokea ulimwenguni.

"Asilimia 85 ya vifo hivi vinatokea kwenye nchi zetu maskini, robo tatu ya vifo vinatoka kwenye uchumi wa hali ya chini, asilimia zaidi ya 80 ya magonjwa haya yanaweza kutibika," alisema.

Aliwataka wanaofunga, wakati wakifuturu na kuona dalili za kuchoka kupitiliza, kupumua kwa shida, kupata kiungulia au kuumwa sehemu ya chembe ya moyo waende hospitali kupata ushauri wa daktari.


NHC
TUNAJENGA TAIFA LETU

## TAARIFA YA UHAKIKI WA WAPANGAJI

Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) linapenda kuutaarifu umma na wapangaji wetu kuwa baada ya zoezi la kuhakiki wapangaji katika Mkoa wa Dar es Salaam kukamilika, sasa zoezi hilo linaendelea kuanzia mwezi Mei 2021 katika Mikoa mingine nchini. Lengo la Uhakiki huu ni kuendelea kuboresha taarifa na mwenendo wa upangaji katika nyumba za Shirika ili kurahisisha utoaji wa huduma kwa wapangaji.

Ili kuwezesha zoezi hili kufanyika kwa ufanisi kila mpangaji anatakiwa kuwa na nyaraka zifuatazo:

1. Mkataba wa upangaji au mkataba wa umiliki wa sehemu ya jengo (long term lease)
2. Nakala/kivuli cha kitambulisho cha ajira (kwa wale wanaoishi kwenye nyumba ambazo zimepangishwa kwa jina la Kampuni)
3. Nyaraka za usajili wa biashara.
4. Nakala ya kitambulisho cha Taifa
5. Picha ndogo 2 (Passport size)

Shirika linaomba ushirikiano kutoka kwa wapangaji wote ili kufanikisha zoezi hili.

**IMETOLEWA NA: KITENGO CHA HABARI NA UHUSIANO**
**SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFA.**

SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFA
MAKAO MAKUU S.L.P 2977 | DAR ES SALAAM TANZANIA | SIMU: +255 22 2105001-5 | NUKUSHI: +255 22 2105000
BARUA PEPE: dg@nhctz.com | TOVUTI: www.nhctz.com



ITV

USIKOSE KUFUATILIA TAMTHILIA YA
UZALO




KUANZIA 3/05/2021 SAA 1:30 USIKU

Ni tamthilia kali, yenye msisimko wa kipekee kutokea Afrika Kusini ikisheheni waigizaji mahiri kama Leleti Khumalo aliyeigiza filamu ya Sarafina.
Watoto wawili wachanga wanabadilishwa vitanda na wahudumu wa hospitali na kila mzazi kupewa mtoto asiye wake bila kujua.
Familia hizi moja ikiongoza genge la uhalifu mkubwa nayapili ikitumikia kanisa zinakuja kuwa na uadui mkubwa baada ya suala la watoto hawa kugundulika.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tahadhari dhidi ya corona muhimu

**TAARIFA** mbalimbali duniani zinaeleza kuwa aina mpya ya kirusi cha COVID kimeibuka nchini India, na tayari mamia ya wananchi wamefariki, huku hospitali kuzidiwa na wagonjwa na huduma ya hewa safi ikikosekana.

Habari katika vyombo vya habari vya kimataifa zinaonyesha jinsi nchi hiyo inavyohangaika kukabiliana na mlipuko huo, huku wananchi wakionekana wakichoma miili ya ndugu zao kama utaratibu wao wa mazishi, ikwamo kuwapo kwa katazo la kusafirisha miili ili kuepuka kusambaa kwa ugonjwa huo.

Tanzania siyo kisiwa kama ambavyo Rais Samia Suluhu Hassan, amesema wakati akiwaapisha makatibu wakuu, na ndiyo maana aliunda kamati maalum ya wataalamu kufanya uchunguzi ili kujua namna Tanzania itakavyo likabili suala hilo.

Tayari tunaona serikali imeimarisha ukaguzi, upimaji na ulinzi katika viwanja vya ndege na mipakani huku hofu kubwa ikiwa ni uhusiano baina ya Tanzania na India na uwapo wa safari za ndege kutoka na kuja nchini.

Tayari Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL), limesitisha safari za India, hadi hapo hali itakapotengamaa nchini humo.

Machi, mwaka jana, kwa mara ya kwanza Tanzania ilirekodi kisa cha kwanza cha mgonjwa wa corona, na hali ilitulia baadaye, na mwaka huu Februari hadi Machi ilijirudia tena, na serikali ilieleza kuwa kuna changamoto ya upumuaji na wananchi kutakiwa kutumia dawa za asili ikiwamo kujifukiza.

Kwa kuwa Tanzania siyo kisiwa tunaona ni muhimu kujipanga kwa kuhamasisha wananchi kuchukua tahadhari za kujikinga ikiwamo uvaaji barakoa, kunawa mikono na kuepuka misongamano kwa kuacha safari zisizo za lazima.

Ni muhimu pia huduma za afya zikaimarishwa na kuhakikisha zinapatikana ikiwamo mahitaji yote ya msingi ya kukabiliana na corona, ili kuepusha madhara kuwa makubwa kwa kujipanga vyema kukabiliana na hali.

Tanzania inapakana na nchi za Kenya, Uganda, Congo, Burundi, Rwanda Msumbiji, Malawi na Zambia na kote huko shughuli za kiuchumi za watu kuingia na kutoka nchini zinazoendelea, kwenye mipaka hiyo kuna uwezekano wa ugonjwa huo kuingia nchini.

Ni muhimu elimu kwa umma ikaanza mapema, na kama Rais Samia alivyotaka kila mmoja kujilinda, basi jitihada zifanyike kuanzia ngazi ya mtaa hadi mkoa, kuhamasisha wananchi kujilinda ili kuepuka uwezekano wa kusambaa kwa ugonjwa huo ikiwa utaingia nchini.


Tayari Chama cha Madaktari Tanzania (MATI), kimetoa angalizo kwa serikali kwamba kuna uwezekano mkubwa kwa baadhi ya watu vipimo vyao kuonyesha kuwa hawana ugonjwa huo wakati wana dalili zote.

Kwa hali hiyo, hata kazi ya kupima kabla na baada ya kuingia nchini inaweza isisaidie sana kwa kuwa kirusi kinaweza kisionekane, ni muhimu kama nchi kujikinga na kuepuka uwezekano wa kutokea maangamizi.

Hakuna ubishi kuwa corona ni hatari na India imeelemewa, zipo nchi zimepoteza wapendwa wao wengi, lakini zipo ambazo hazijarekodi kisa chochote kutokana na kuchukua tahadhari zote muhimu ikiwamo kuvaa barakoa, kuepuka misongamano, kunawa mikono mara kwa mara.

Suala la afya ni la mtu binafsi, ni muhimu jitihada za kujikinga zikafanywa na mtu binafsi ili kuepuka kupotea kwa nguvu kazi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Bajeti ya elimu iwe kwetu sote



Na Yasmine Protace

WIKI hii tumeshuhudia kusomwa Bajeti ya Wizara ya Elimu na Ufundi, ikipitisha zaidi ya shilingi trilioni moja katika matumizi yake kwa kipindi cha mwaka mmoja ujao wa fedha, 2021/2022.

Wizara ilitaja vipaumbele vyake mbalimbali ambavyo vimeboreshwa katika bajeti, huku ikipokewa na wanajamii kwa mitazamo tofauti waliotoa mapendekezo yao.

Profesa Joyce Ndalichako, waziri mwenye dhamana na elimu nchini, anasema mpango wa bajeti umezingatia Dira ya Taifa, pia maoni ya wadau wa elimu kitaifa katika mustakabali mpana wa maslahi ya taifa.

Anasema mapitio ya elimu yatazingatiwa ili kuendana na kasi iliyopo sasa, serikali ikizingatia masomo ya ujuzi, ili yaweze kuwasaidia wanafunzi wa shule za msingi na sekondari zilizopo.

Selemani Bishagazi, aliyeshiriki Semina za Jinsia na Maendeleo (GDSS) zinazoratibiwa na TGNP Mtandao, ana mapendekezo kwamba, inapowezekana ni muhimu shule za msingi na sekondari ziwe na elimu, pia ujuzi stahiki kumsaidia mwanafunzi amudu hitaji la kujiajiri.

Katika uhalisia unaotawala sasa, ni kawaida na rahisi kwa mtoto akamaliza elimu ya ama darasa la saba au kidato cha nne, bado anakosa umahiri wa kujiajiri.

Ina maana, hata katika ngazi ya juu zaidi nayo inakuwa mtihani katika suala la kujiajiri, mathalan vyuoni vya Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) ili apate stadi hiyo, hata kufika hatua ya ujuzi kama wa kushona nguo, kuranda mbao, kupika, ujenzi au ujasiriamali.

Mtazamo wa umma unawaangukia hata wabunge wawakilishi wa sehemu mbalimbali, nao hata kabla hawajaenda bungeni, kuna umuhimu wa kuwasikiliza mawazo ya wapigakura, ili yaingizwe bungeni.

Zainabu Mmari, ni mfanyakazi wa asasi inayojihusisha na utetezi wa kijinsia ya TGNP Mtandao, anasema kuwa mapitio ya sera ya elimu ni jambo jema na kama wanaharakati watapatiwa ushirikiano, kufikia hatua inafanyiwa kazi hadi kuachwa ilete matunda kwa umma.

> **Zainabu Mmari, ni mfanyakazi wa asasi inayojihusisha na utetezi wa kijinsia ya TGNP Mtandao, anasema kuwa mapitio ya sera ya elimu ni jambo jema na kama wanaharakati watapatiwa ushirikiano, kufikia hatua inafanyiwa kazi hadi kuachwa ilete matunda kwa umma.**

Hapo wanaipongeza Wizara ya Elimu na Ufundi, kwa utoaji misamaha ya tozo za mikopo ya kielimu, jambo lililokuwa linawaumiza zaidi kiuchumi.

Hawa Juma, anasema elimu ya ujuzi izingatiwe na izae matunda kwa wanafunzi waliopo shule za msingi na sekondari, waweze kujiajiri pindi wanapomaliza masomo yao katika ngazi tofauti.

"Kwa sasa ajira inasumbua, lakini kuwapo elimu ya ujuzi kutasaidia wahitimu kujiajiri wenyewe na sio kutegemea kuajiriwa," anasema, akiungwa mkono na Monica John mfanyakazi mwingine kutoka TGNP Mtandao.

Huyo anaangukia katika ushauri kwamba, kwa sasa kinachotakiwa kufanyika ni wanaharakati kushirikiana na wanajamii wanaoishi nao, wapitie bajeti zinazotolewa na hapo itakuwa rahisi kujua maoni ya kila mmoja, ambayo ni vyema yawasilishwe kwa wahusika yafanyiwe kazi.

Ibrahim Aweso, mwanaharakati na mdau wa Semina za Jinsia na Maendeleo, anakiri kufuatilia bajeti ya elimu ameielewa, akiwa na ufafanuzi kwamba kipengele cha utafiti wa kielimu, zimeshaanza kufanywa na wataalamu kutoka vyuoni, ambazo zinatakiwa kuleta matunda.

Anasema, katika bajeti hiyo hakusikia kipengele cha elimu bure ikizungumziwa eneo analoliona la kipaumbele, ihali mwaka ujao idadi ya wanafunzi katika shule za msingi na sekondari inatarajiwa kuongezeka maradufu.

Eneo lingine la malalamiko linasimamia majengo, pia hakusikia upande wa watoto ngazi ya chekechea.

HABARI KITAIFA




Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mwita Waitara, akizungumza wakati wa ufunguzi wa mkutano wa Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB) na makandarasi wazalendo jijini Arusha. Wengine ni Makamu Mwenyekiti wa Bodi, Joseph Tango (wa pili kushoto), Msajili wa bodi, Injinia Rhoben Nkori na Mwenyekiti wa bodi, Injinia Consolatha Ngimbwa. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Serikali yakemea ubinafsi makandarasi

**Na Joseph Mwendapole,** ARUSHA

SERIKALI imewataka makandarasi wazalendo kuacha ubinafsi na kuungana ili kuwa na uwezo wa kutekeleza miradi mikubwa ya ujenzi.

Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mwita Waitara, alisema hayo jana wakati akifungua mkutano wa makandarasi wazalendo ulioandaliwa na Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB) unaoendelea jijijini hapa.

Alisema serikali inatamani kuona kazi kubwa na zinazotumia fedha nyingi zinafanywa na makandarasi wazalendo ili fedha hizo zibaki nchini.

"Hakuna kiongozi wa serikali anayefurahia kuona kazi za miradi mikubwa ya ujenzi zinafanywa na makandarasi wa nje. Yaani tunatafuta fedha kwa shida halafu zinakwenda kwa kampuni za nje? Hapana," alisema.

Naibu Waziri alisema makandarasi wazalendo wakiungana na kufanya miradi mikubwa, fedha zinabaki nchini na kufanya shughuli mbalimbali ambazo zinasaidia kuchochea maendeleo.

Alisema haifurahishi kuona makandarasi wazalendo wakiendelea kufanya kazi ndogo ndogo na wakitumiwa na makandarasi wa nje kufanya 'subcontract' wakati nchi ina wataalamu wa kutosha.

Waitara alisema alitembelea baadhi ya miradi na kukuta zaidi ya asilimia 90 ya wataalamu wanaotekeleza miradi ni wazalendo wanaotumiwa na kampuni za nje.

"Nilishangaa nilipotembelea mradi mmoja Tanga nikakuta wataalamu wote ni Watanzania na Wachina walikuwa wawili tu. Sasa kama ni hivyo kwa nini tusifanye wenyewe, kikubwa acheni ubinafsi," alisema.

Naibu Waziri alisema serikali itafurahi kuona miradi mingi mikubwa ikifanywa na kampuni za wazalendo huku kampuni za kigeni zikipewa kazi (subcontract) na kampuni za Watanzania.

"Tukiacha ubinafsi tunaweza kabisa kwa sababu unakuta kampuni za wazalendo wakiungana fedha zikiingia tu kwenye akaunti kila mtu anaanza kuwaza nyumba mpya, gari zuri suti mpya na tai. Sasa haya lazima tuyaache tufanye kazi kwanza," alisema.

Kuhusu utaratibu wa 'force account' ambao umekuwa ukitumiwa na serikali kutekeleza miradi, Naibu Waziri alisema serikali iliamua kufanya hivyo kutokana na ubabaishaji wa baadhi ya makandarasi.

Alisema kama wataihakikishia serikali kwamba watatekeleza miradi hiyo kwa ubora, kwa wakati na kwa gharama ndogo iko tayari kufanya mabadiliko.

"Hili la force account linazungumzika kwa sababu vitu rahisi wakati mwingine navyo huwa vinakuwa ghali sana na Waziri atalitolea tamko hili kwenye mkutano wenu wa Mwanza," alisema.

Akizungumzia rushwa, Waitara alisema imekuwa tatizo kwani makandarasi wanapotoa rushwa wamekuwa wakishindwa kukamilisha miradi.

"Unakuta mkandarasi anapewa mradi kwa ujanja ujanja tu lakini hana uwezo wa kukamilisha mradi kwa wakati na kwa ubora. Unakuta hana vifaa, hana fedha, hana ujuzi unaotakiwa mwisho wa siku mradi unamshinda," alisema.

Mwenyekiti wa CRB, Mhandisi Consolata Ngimbwa, aliiomba serikali iwape miradi makandarasi wazalendo badala ya kujenga yenyewe kwa kutumia utaratibu wa 'force account'.

Alisema utaratibu huo umewaweka kwenye hali ngumu makandarasi wazalendo kwa kuwa wamekaa muda mrefu bila kazi wakati wengine wana mikopo.

Ngimbwa aliungana na Naibu Waziri kuwataka makandarasi waache ubinafsi na kuungana ili kupata mitaji ya kufanya miradi mikubwa ya ujenzi badala ya kutegemea kazi ndogo.

# DC: Wanawake msidharau waume zenu kwa pesa

**Na Zuhura Zukheir,** MUFINDI

IMEDAIWA kuvunjika kwa ndoa nyingi kunatokana na wanawake kudharau waume zao baada ya kipato kuongezeka hali inayosababisha ongezeko la watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi.

Mkuu wa Wilaya ya Kilolo, Asia Abdallah, alisema hayo wakati akifungua warsha ya fursa kwa wanawake katika misitu wilayani Mufindi iliyofanyika Chuo cha Mafunzo ya Mazao ya Misitu kwa vijana cha panda miti kibiashara, na kuwataka watumie fursa za kiuchumi wanazozipata kuheshimu waume zao na kulinda haki za watoto.

Asia alisema kuwa wanawake wengi wanapopanda kiuchumi wamekuwa wakileta dharau kwa waume zao hali inayosababisha migogoro ya kindoa ambayo mwisho wake huwa ni kutengana na athari kubwa huangukia kwa watoto kukosa malezi ya baba na mama.

"Ninaomba niongee na wanawake wote wa wilayani Mufindi kipindi mnapokuwa uchumi wenu upo chini mnakuwa watulivu na wenye kujali familia serikali inataka wanawake wote mpande kiuchumi, lakini mnatuangusha sisi wanawake wenzenu pale mkishapanda tu kiuchumi mnaanza kumdharau baba nyumbani, haipendezi tunawaathiri kisaikolojia hawa watoto wetu wanaposhuhudia migogoro kila siku, naomba tusijisahau katika ndoa zetu," alisema Asia.

Alisema kujishughulisha kwa mwanamke na kupata kipato chake mwenyewe ni kwa ajili ya kumsaidia mumewe kuhudumia familia na sio kumpanda kichwani kwa sababu naye ana uwezo wa kufanya kazi.

Aliwataka wanawake hao kutumia fursa ya misitu kujipatia kipato kwa kujishughulisha kama kufuga nyuki, kulima miti, na kufanya biashara ya miche kwa ukanda wa Nyanda za Juu Kusini unategemewa kwa zao la miti nchini.

Mratibu wa pandamiti kibiashara kongani ya Mafinga, Nyachia Robert, alisema warsha hiyo imelenga kuwajengea uwezo na kuwaonesha kinamama fursa zilizomo katika sekta ya misitu na jinsi ya kuzitumia kujiletea maendeleo.

Nyachia alisema mradi huo misingi yake imejengwa katika haki za binadamu kumwezesha mwanamke ambaye kwa namna moja ama nyingine hajonekana na kwa kutokuoneka amekosa fursa kutumia fursa zilizopo katika sekta za misitu.

Alisema ukiwaunganisha kinamama pamoja wana uwezo kujielezea changamoto zao kwa kujiamini zaidi kuliko kuwachanganya na wafanyabiashara wanaume kwa kuwa hujihisi hawana nafasi ya kujenga hoja.

Mmoja wa washiriki, Euzabia Sanga, kutoka wilayani Mufindi alisema kupitia warsha hiyo wamejifunza jinsi ya kutumia mitandao ya kijamii kutafuta masoko na fursa katika biashara zao badala ya kukaa wakisubiri wateja ambao hawajui watakuja lini.



# Asilimia 90 ngozi haina viwango bora

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

ASILIMIA 90 ya ngozi zinazozalishwa nchini na kupelekwa viwandani kutengeneza bidhaa mbalimbali hazikidhi viwango vya ubora.

Hayo yalibainishwa jana jijini Mwanza na Kaimu Katibu Tawala Mkoa wa Mwanza, Emmily Kasagala, wakati akifunga mafunzo ya kuwajengea uwezo wakaguzi 33 wa ngozi kutoka mikoa ya Kanda ya Ziwa.

Alisema kwa sasa kuna viwanda viwili ambavyo vina uwezo wa kusindika futi za mraba 10,000 hadi 15,000 za ngozi na kwamba kwa siku vipande vya ngozi ya ng'ombe 1,000 na mbuzi 9000 huzalishwa.

Hata hivyo Kasagala alisema asilimia 90 ya ngozi inayokosa ubora inawasababishia hasara wafanyabiashara na wenye viwanda.

Kutokana na hali hiyo, alisema tatizo la viwanda kukosa malighafi yenye viwango vinavyotakiwa, linapaswa kufanyiwa kazi ili kuhakikisha kunakuwa na uchumi wa kati unaotegemea viwanda

Aliongeza kuwa serikali inatekeleza mikakati ya kuendeleza sekta hiyo hapa nchini.

Licha ya Tanzania kuwa ya pili kwa uzalishaji wa ngozi, kuna upotevu wa bidhaa hiyo, hivyo wasimamizi wa sekta ya ngozi kupitia mafunzo hayo watapata uwezo wa kuisimamia.

Kaimu Mkurugenzi Msaidizi wa Mazao ya Mifugo, Usalama wa chakula na Lishe katika wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Gabriel Bura, alisema wakaguzi hao wanatoka mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Mara na Simiyu.

Alisema lengo la mafunzo hayo ni kuongeza usimamizi wa sheria ya biashara ya ngozi, uhifadhi na kusimamia ubora wa bidhaa hiyo, ili kuhakakikisha kiwango cha ubora wa ngozi kizipanda kutoka asilimia 10 iliyopo sasa hadi 80 ifikapo mwakani.

# WMA yaonya wafanyabiashara kupunja wateja

**Na Mwandishi Wetu,** SONGEA

WAKALA wa Vipimo (WMA) imewataka wafanyabiashara kujiepusha na vitendo vya kuchezea vipimo kwa lengo la kujipatia faida zaidi na kuonya kuwa wanaofanya hivyo watakumbwa na adhabu kali

Meneja wa WMA Mkoa wa Ruvuma, Nyagabona Mkanjabi, alisema hayo jana wakati wa mafunzo na elimu kwa umma kuhusu matumizi sahihi ya vipimo na ufungashaji kwa wafanyabiashara wa mkoa wa Ruvuma yaliyofanyika katika ukumbi wa Manispaa ya Songea, mjini hapa.

Alisema kuchezea vipimo ni kinyume cha Sheria ya Vipimo Sura Na. 340 na mapitio yake mbalimbali na kwamba adhabu kwa mtu atakayekutwa amechezea vipimo ni faini isiyopungua Sh. 100,000 na isiyozidi 20,000,000 kwa kosa.

Mkanjabi alitaja madhara mbalimbali yatokanayo na matumizi yasiyo sahihi ya vipimo kuwa ni pamoja na kukiuka Sheria ya Vipimo ambayo inaweza kusababisha mfanyabiashara kuadhibiwa kwa kulipa faini au kupata adhabu ya kifungo mahakamani na mali yake kutaifishwa.

Alisema kumpunja mteja ni wizi na ni kinyume na maandiko ya vitabu vitakatifu, lakini vilevile biashara zinaweza kufa au kufilisika kwa kuzidisha bidhaa kwa wateja pasipo kutumia vipimo vilivyo sahihi katika biashara.

Mshiriki wa mafunzo hayo, John Bura ambaye ni mfanyabiashara wa gesi Songea aliipongeza WMA kwa kuwapatia elimu ya matumizi ya vipimo sahihi kwa kuwa itawasaidia kuepuka kujipunja na kuwapunja wateja na kuhakikisha wanatumia mizani katika uuzaji na ununuzi wa bidhaa.

Mkuu wa Wilaya ya Songea mkoani Ruvuma, Pololet Mgema, alitaka WMA kutoa mafunzo zaidi ya matumizi sahihi ya vipimo na namna bora ya kuzingatia ufungashaji sahihi wa bidhaa.

Aliipongeza WMA kwa kuelimisha wafanyabiashara, wajasiriamali na wakulima wa mkoa wa Ruvuma huku akiitaka iendelee kuwasaidia wafanyabiashara kwa kuwapa elimu ya vipimo mara kwa mara na kufanya ukaguzi wa kushtukiza ili kujiridhisha kama vipimo vinatumika kwa usahihi.

Mgema pia aliipongeza WMA kwa kuongeza na kupanua wigo wa kazi za vipimo katika maeneo mapya ambapo kwa sasa taasisi hiyo inafanya uhakiki wa dira za maji pamoja na mita za umeme.

Aliagiza mamlaka zote za maji Mkoa wa Ruvuma kuhakikisha wateja wote wanafungiwa mita za maji zilizohakikiwa na WMA.




Mkuu wa kitengo cha kudhibiti majanga ya kibiashara wa Benki ya Afrika (BOA), Soud Ali (kushoto), akikabidhi msaada wa vyakula mbalimbali kwa Mkurugenzi wa kituo cha kulea yatima cha Amani Foundation for orphanages cha Kibunguni Kigamboni mkoani Dar es Salaam, Hajjat Zubeida Abdallah, vilivyotolewa na benki hiyo kwa ajili ya futari kwa watoto yatima 58 wanaolelewa kituoni hapo, jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# PAC yataka makandarasi wabanwe

**Na Zuhura Zukheir,** IRINGA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) imeiagiza Wizara ya Nishati kuwasimamia makandarasi wanaotekeleza miradi ya umeme vijijini ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma kwa wakati.

Maagizo hayo yalitolewa juzi baada ya PAC kutembelea Kijiji cha Holo, wilayani Iringa mkoani Iringa na kupokea malalamiko ya wananchi ambao walemilipia fedha kuunganishiwa umeme lakini bado hawajapata huduma hiyo.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Holo, Winston Mpalanzi, alisema licha ya kufikisha umeme katika kijiji hicho, baadhi ya vitongoji na kaya hazijafikishwa huduma ya nishati katika miradi inayotekelezwa na Wakala wa Nishati Vijijini (REA), hali inayoendelea kuzua maswali kwa wananchi.

Pamoja na malalamiko hayo, PAC ilielezea kuridhishwa na utendaji kazi wa Wizara ya Nishati katika suala zima la kuwapelekea wananchi umeme vijijini kwa gharama nafuu kupitia mradi wa REA na kutoa maagizo kadhaa ambayo yanatakiwa kufanyiwa kazi.

Akizungumza baada ya ziara hiyo, Mwenyekiti wa PAC, Naghenjwa Kaboyoka, alisema kwa kiasi kikubwa wizara imefanya kazi kubwa ya kupeleka umeme vijijini na kuwaongezea kasi ya kufanya shughuli za kimaendeleo.

Alisema wametembelea kijiji cha Holo na kubaini kuwa kwa asilimia kubwa wananchi wamepatiwa umeme licha ya baadhi ya vitongoji na kaya kutopatiwa huduma hiyo jambo ambalo linaweza kushughulikiwa na wizara kwa sababu liko chini ya uwezo wao.

Licha ya kazi nzuri inayofanywa, PAC imeiagiza wizara kuhakikisha inawasimamia watendaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) ili kuwahudumia wananchi ambao wanahitaji huduma hiyo kwa ajili ya maendeleo yao na nchi kwa ujumla.

Kaboyoka alisema makandarasi wengi wamekuwa wanafanya kazi kinyume cha mikataba yao, hivyo ni lazima wizara ikahakikisha inawasimamia vilivyo ili kuhakikisha fedha za serikali hazipotei.

Pia aliitaka Wizara ya Nishati kuhakikisha inasimamia vilivyo mapato ya wananchi kwa kuhakikisha kila kazi inayofanywa na watendaji na makandarasi inaendana na gharama za kazi iliyofanywa na si vinginevyo.

Kamati hiyo pia iliitaka TANESCO kuhakikisha inafanya kazi kwa weredi ili kuondoa makandokando ambayo yamekuwa yanajitokeza mara kwa mara katika shirika hilo.

Naye Naibu Waziri wa Nishati, Stephen Byabato, alisema wamepokea maagizo yote yaliyotolewa na kamati na kwamba watayafanyia kazi huku akisema maagizo mengine yameshafanyiwa kazi.

Byabato alisema serikali imetumia zaidi ya Sh. bilioni 30 kupeleka umeme wa REA katika vijiji na vitongoji vya mkoa wa Iringa na hadi kufikia Desemba, mwakani, vijiji na vitongoji vyote vitakuwa vimepata umeme.

Alisema katika mkoa wa Iringa wenye vijiji 354, asilimia kubwa vijiji vimepata umeme isipokuwa 31 ambavyo vinatarajia kupata umeme kabla ya wakati uliopangwa.

## Wanafunzi wa kilimo kunolewa kwa vitendo

**Na Mwandishi Wetu, MWANZA**

KAMPUNI ya Bia ya Serengeti Breweries Limited (SBL) imesema imejizatiti kuwapa wanafunzi nyenzo na mafunzo zaidi ya kivitendo kama njia mojawapo ya kuongeza idadi ya wataalamu wa kilimo nchini.

Haya yalisemwa na Mkurugenzi Mtendaji wa SBL, Mark Ocitti katika wakati wa kuwapongeza wanafunzi 17 waliopata nafasi za ufadhili kupitia programu hii kutoka Chuo cha Igabiro Training Institute of Agriculture kilichoko mkoa wa Kagera.

SBL imelenga kufanya haya kupitia programu hii maarufu inayojulikana Kilimo Viwanda inayolenga kusaidia wanafunzi kutoka familia maskini ili waweze kusomea masomo ya kilimo kwenye ngazi ya diploma katika vyuo vya ndani.

Ocitti alisema: "Programu ya Kilimo-Viwanda inawajengea wanafunzi uwezo wa kuelewa kimatendo, ambao ni mfumo nje ya mafunzo yao ya kila siku darasani, mfano kutembelea viwanda vyetu vya bia na mashambani." Ocitti alifafanua kuwa ufadhili huu unajumuisha malipo yote ya chuo na gharama zingine katika kipindi chao chote cha masomo."

Kadhalika, Ocitti alisema kuwa programu hii imedhamiria kuongeza nguvu juhudi za serikali katika kuongeza wataalamu zaidi wa kilimo nchini. SBL

Kampuni hiyo inafanya kazi na mtandao wa wakulima 400 kwenye mikoa nane nchini ambapo wananunua nafaka kwa ajili ya uzalishaji bia. SBL inatumia takribani tani 17,000 sawasawa na asilimia 70 na mahitaji yao kwa mwaka. Programu hii iliyoanzishwa mwaka 2020 imesaidia wanafunzi 70 kusomea kozi za diploma katika ujuzi wa kilimo katika vyuo vingine vitatu ambavyo ni Kaole Wazazi College of Agriculture (Bagamoyo), Kilacha Agriculture Training Institute (Moshi) na St. Maria Goretti Agriculture Training Institute (Iringa).

Mkuu wa Chuo cha Igabiro Training Insitute of Agriculture, Sadock Stephano, aliipongeza SBL kwa msaada wao wa dhati na kusisitza kampuni mengine waige mfano katika kuwasaidia wanafunzi kutoka familia maskini nchini.

# Kaya zajenga zahanati kuwakomboa wajawazito

**Na Beatrice Moses**

WAKAZI wa Mtaa wa Saranga Wilaya ya Ubungo, Dar es Salaam, wamekubaliana kuchangishana Sh 10,000 kila kaya ili kujenga jengo la zahanati lenye huduma ya kliniki ya watoto na wajawazito.

Hatua hiyo ikifanikiwa inatajwa kuwa itawapa ahueni wajawazito na kinamama wanaopeleka watoto kliniki kwa kuwa wanapata huduma hiyo chini ya mti wa mkwaju uliopo nje ya ofisi ya Serikali ya Mtaa huo.

Katika mkutano uliofanyika juzi na kuhudhuriwa na wananchi kadhaa Mwenyekiti wa Mtaa wa Saranga, Godwin Muro, alibainisha kuwa kutokana na mazingira yalivyo, badhi ya huduma kwa wajawazito zinatolewa kwenye ofisi yake.

" Wapo wanaojiuliza maswali, kitanda kile ofisini kwangu huwa nakitumia kujipumzisha ! leo nawafahamisha kile kinatumika kuwahudumia wajawazito, nawasihi tuongeze bidii ya kutoa michago ili tukamilishe ujenzi wa zahanati kama ulivyokubaliana awali," alisema Muro,

Aliongeza: "Huduma hiyo ni muhimu inapaswa kutolewa kwa utulivu tunapaswa kufanya kitu hatuwezi kuisubiri Serikali, fedha kutoka kwenye mfuko wa jimbo tunaweza kusaidiwa iwapo tutafanikiwa kufunga linta, "alisema.

Alibainisha kuwa hadi sasa mchango iliyotolewa ni Sh. 8,000,000 ambazo zimetumika katika kuanza kujenga msingi wa jengo hilo linalokadiriwa kugharimu shiligi milioni 110.

Alisema kuwa anaamini kuwa wakazi wa eneo hilo wakiwa na nia moja na wakiunganisha nguvu za hali na mali itawezesha jengo la zahanati walilokusudia kulijenga lenye vyumba vitatu na maabara litakamilika, hivyo kuwezesha huduma za afya kutolewa kwenye mazingira mazuri.

Mtendaji wa Mtaa huo, Edwin Misana, aliwaeleza wananchi kuwa michango hiyo inakusanywa kwa utaratibu baada ya kuruhusiwa na halmashauri, hivyo kila mwananchi atakayechangia atapewa risiti yake ili kuweka kumbukumbu vyema .

Mmoja wa wakazi wa eneo hilo, mzee Leoford Bakuza, alipongeza juhudi hizo, pia akashauri pamoja na ujenzi huo, ni vyema viongozi wakaangalia pia namna nzuri ya kuboresha barabara kwa kuwa zimeharibika hivyo kuwa kero hata kuhatarisha wagonjwa na wajawazito.

Wakazi wa Mtaa wa huo wamekuwa wakitibiwa kwenye Kituo cha Afya cha Kimara, ambacho kinahudumia wananchi kutoka kwenye mitaa tisa ya Kata ya Saranga.

## Taasisi yawakubali wanahabari wanawake

**Beatrice Shayo na Lulu George,** NAIROBI

WAANDISHI wa habari wanawake wametajwa kuwa na uwezo mkubwa licha ya kutokupewa nafasi katika vyombo vya habari ikiwamo kwenye ngazi za kutoa uamuzi.

Hayo yalisemwa na Ofisa Mipango wa Taasisi ya Friedrich Naumann Foundation for Freedom, Veni Swai, wakati wa mafunzo ya wiki moja yaliyowashirikisha waandishi wa habari wanawake kutoka Tanzania na Kenya.

Alisema mafunzo hayo yamelenga kuwajengea uwezo waandishi wa habari wanawake ili watambue nafasi zao na kufikia malengo katika kushika nafasi za uongozi.

Swai alisema wamekuwa wakifanya shughuli mbalimbali ikiwamo kuwajengea uwezo wadau yaani wanasiasa, vijana, wanawake na kuangalia masuala ya haki za binadamu.

Alisema wanapokuwa wanafanya kazi hizo wamegundua jambo ambalo limewagusa kufanya kazi na waandishi wa habari kwa sababu ili uweze kupata jamii inayoweza kufanya uamuzi sahihi ni vizuri iwapo taarifa sahihi.

"Tukagundua ili upate taarifa sahihi inatupasa kufanya kazi na vyombo vya habari. Tulipofanya kazi na waandishi tuligundua wanawake wachache wameshiriki katika mafunzo ambayo yalikuwa ni jukwaa linalotoa nafasi kwa waandishi kujisemea mambo mbalimbali ambayo yamewapata ikiwamo kupoteza ajira kutokana na mlipuko ugonjwa wa Corona," alisema.Swai alisema wanawake wachache walishiriki licha ya kupatiwa taarifa na wengine walikuwa na visingizio.

Alisema hata walipotoa fursa ya kwenda kuhudhuria mafunzo Ujerumani walishiriki wachache wakaona walifanyie kazi suala hilo na kutafuta njia ya kuwawezesha waandishi wa habari wanawake ili waeleze sababu ambazo zinawakwamisha.

"Hili ni moja ya vitu ambavyo vilitusababisha kufanya mafunzo haya na kazi nyingine ambazo tunazozifanya, tumekuwa tukifanya masula ya haki za binadamu, tumejikuta tunakutana na mambo mbalimbali tukielezwa waandishi wanawake wanapitia matatizo, tukaona tuwakutanishe ili waongeze na kutambua nafasi zao," alisema.

Aidha, Swai alisema mwandishi wa habari mwanamke ana nafasi kubwa ya kulizungumzia jambo kwa upana zaidi kwa sababu ni sehemu ya jamii na pia ni kiongozi katika familia.

Kwa upande wake mwalimu wa mafunzo, Njeri Kabeberi, alisema ni muhimu kubadilisha mfumo wa kufanya kazi kwa kuweka malengo na kutafuta fursa kubwa badala ya kufanya kazi hiyo kwa mazoea.

Alisema unapofanya kazi kwa malengo kuna mambo makubwa hujitokeza ikiwamo uwezo wa kazi kuonekana na kupanda daraja kazini.

# NOTISI/ TANGAZO

**JY AUCTIONEERS CO.LTD, NUTMEG AUCTIONEERS AND PROPERTY MANAGERS CO.LTD, SALEI AUCTION MART,REAL MASTER COMPANY LTD, WAUNGWANA AUCTION MART,MASETO AUCTIONEERS,BEST GROUP LTD,TAUSI AUCTION MART NA MASHOKA AUCTION MART** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya benki ya AKIBA COMMERCIAL BANK PLC, tunatoa notisi ya kulipa madeni kwa wadaiwa wafuatao ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili,Vinginevyo, tutafanya minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| NA | JINA LA MDAIWA | TAWI ALILOKOPA | JINA LA MWENYE DHAMANA | AINA YA DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE NA SAA YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | RASHID ATHUMAN MWEDI | DODOMA | RASHIDATHUMAINIMWEDI | NYUMBA | HOMBOLO | 23/05/2021 NA KUENDELEA KUANZIA SAA.3:00 AHSUBUH |
| 2 | VICTOR MOSSES NNKO | DODOMA | VICTORMOSSESNNKO | NYUMBA | KIBAIGWA-MAJENGO | 21/05/2021 NA KUENDELEA KUANZIA SAA.3:00 AHSUBUH |
| 3 | TITO KALAMU SANGA | DODOMA | TITO KALAMU SANGA | NYUMBA | KIBAIGWA - MAJENGO | 21/05/2021 NA KUENDELEA KUANZIA SAA.3:00 AHSUBUH |
| 4 | HULDA FRANK KOMBE | ARUSHA | ESTER POLIKARIO URIO | NYUMBA | KITENGARE-KATA YA KIMANDOLU | 21/05/2021 NA KUENDELEA KUANZIA SAA.3:00 AHSUBUH |
| 5 | FLUGENCE GERVAS KIMARIO | ARUSHA | FLUGENCE GERVAS KIMARIO | NYUMBA | KATA YA SOKONI-MTAAWAMADUKANI | 23/05/2021 NA KUENDELEA KUANZIA SAA.3:00 AHSUBUH |
| 6 | JULIUS KALANGA LAIZER | ARUSHA | JULIUS KALANGA LAIZER | | ENGUTOTO-MONDULI | 29/05/2021 NA KUENDELEA KUANZIA SAA.3:00 AHSUBUH |
| 7 | Ally Miuti Yasini | MBAGALA | Ally Miuti Yasini | NYUMBA | Chamanzi Machimbo | 21/5/2021 Kuanzia saa 4:30 asubuhiya kuendelea |
| 8 | Yunusa Saidi Mlemba | MBAGALA | Yunusa Saidi Mlemba | NYUMBA | Kongowe Mzinga "A" | 21/5/2021 Kuanzia saa 4:30 Asubuhi na kuendelea |
| 9 | Vedastus Salum Ndiratuma | MBAGALA | Vedastus Salum Ndiratuma | NYUMBA | Mwandege Kwa Bi Mafuru | 21/5/2021 Kuanzia saa 6:30 Mchana na kuendelea |
| 10 | Yusuph Ahmad Mnyasi | MBAGALA | Ramadhani Abdalah Kizi | NYUMBA | Kisemvule Mwisho | 21/5/2021 |
| 11 | Elia Machaka Ulema | MBAGALA | Elia Machaka Ulema | NYUMBA | Kigamboni Ungindoni | 22/5/2021 Kuanzia saa 5:00 Asubuhi na kuendelea |
| 12 | Elias Lubadili Makala | MBAGALA | Elias Lubadili Makala | NYUMBA | Mbande Rufu | 22/5/2021 Kuanzia saa 8:00 Mchana na kuendelea |
| 13 | KHALIDI MOHAMED ISSA | ARUSHA | KHALIDI MOHAMEDI ISSA | NYUMBA | OSTERBAY UNGALIMITED ARUSHA | 21/05/2021 KUANZIA SAA 4: 00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 14 | FULGENCE GERVAD KIMARIO | ARUSHA | FULGENCE GERVAD KIMARIO | NYUMBA MBILI | UNGALIMITED ARUSHA | 24/05/2021 KUANZIA SAA 4: 00 ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya nyumba au kiwanja papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2. Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali, hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwishailipa.
3. Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no. 0754497396 /0785242219/ 0754376493
4. Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba, benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi benki bila gharama yeyote.

## Singida Magharibi sasa kupata maji

SERIKALI imekamilisha upatikanaji wa vyanzo vya maji kwa kuchimba visima virefu katika vijiji saba vya jimbo la Singida Magharibi.

Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, aliyasema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Singida Magharibi(CCM), Elibariki Kingu.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji serikali lini itaanza ujenzi wa miundombinu ya maji katika vijiji vilivyopo kwenye jimbo hilo ambavyo utekelezaji wake unasuasua.

Akijibu swali hilo, Waziri Aweso alitaja vijiji hivyo kuwa ni Kipunda, Minyughe, Ighombwe, Makungu, Mpetu, Magungumka na Mnang'ana.

Alikiri serikali inatambua tatizo la upatikanaji wa huduma ya maji katika jimbo hilo na kwamba ili kuendelea kutatua tatizo hilo serikali imekamilisha upatikanaji wa vyanzo vya maji kwa kuchimba visima virefu katika vijiji vya Kipunda, Minyughe, Ighombwe, Makungu, Mpetu, Magungumka na Mnang'ana.

Alibainisha kuwa uendelezaji wa visima hivyo kwa kujenga miundombinu ya usambazaji utaanza mwaka wa fedha 2021/22 ambapo kazi zitakazofanyika ni pamoja ununuzi na ufungaji wa pampu saba, ujenzi wa nyumba za mashine saba.

"Nyingine ni ujenzi wa matanki ya kuhifadhi maji Saba yenye ukubwa lita za ujazo 90,000 na 100,000 ununuzi na ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji umbali wa Kilomita 85.9 na vituo vya kuchotea maji 79," alisema.

Pia, alisema serikali katika mwaka wa fedha 2021/22 imepanga kutekeleza miradi minne ya ujenzi wa miundombinu ya usambazaji maji katika vijiji vya Irisya, Iglansoni, Ihanja na Kaugeri vilivyopo katika jimbo hilo.

Katika swali la nyongeza, Mbunge huyo aliitaka serikali kueleza ni lini itatoa fedha kwa ajili ya ukamilishaji mradi wa maji kwenye kata ya mtunduru na vijiji vya Igombwe ambao umechukua muda mrefu sana kutekelezwa.

Akijibu swali hilo, Aweso alieleza kuwa ndani ya mwezi huu fedha zitatolewa kwa ajili ya ukamilishaji wa miradi hiyo.

# Mfumo wa maombi ya uhamisho TAMISEMI waja

Habari zote na Augusta Njoji, DODOMA




OFISI ya Rais,Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), inatarajia kuzindua mfumo wa kielektroniki wa maombi ya uhamisho ambao utachuja kwa uhakika.

Mfumo utawezesha watumishi katika maeneo ya vijijini kubaki kufanya kazi kwenye maeneo yao bila ya kuhama bila sababu maalum.

Naibu Waziri wa Ofisi hiyo, Dk. Festo Dugange, alitoa kauli hiyo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Korogwe Vijijini (CCM), Timotheo Mzava.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji serikali lini itazingatia ushauri wa Wakurugenzi wa Halmashauri kabla ya kufanya uhamisho wa watumishi.

"Moja ya sababu kubwa ya upungufu wa watumishi kwa halmashauri za vijijini ni wale wanaopangiwa wanaenda kule wakipata ajira wanahama,na TAMISEMI mmekuwa mkipitisha bila ya kuzingatia maoni ya wakurugenzi, Je, ni lini mtazingatia ushauri wao?"alihoji Mzava.

Akijibu, Naibu Waziri huyo alisema Ofisi hiyo pia itaanzisha mikataba ya watumishi wanaoajiriwa katika maeneo ya vijijini ili kuwawezesha watumishi hao kukaa eneo moja kwa muda mrefu na hivyo kuondoa kero iliyopo ya watumishi wanaopangiwa vijijini kuomba uhamisho.

Alikiri kumekuwapo tatizo la upungufu wa watumishi kwenye mamlaka ya serikali za mitaa ikiwamo Korogwe, lakini jitihada zimekuwa zikiendelea kufanyika. "Lakini sio kweli kwamba TAMISEMI imekuwa ikipitisha maombi yote ya uhamisho kwa watumishi wanaohama, mara kwa mara tumekuwa tukichuja sababu za msingi ambazo zinapelekea baadhi kukubaliwa na walio wengi kutokubaliwa kupata," alisema.

Hata hivyo, alisema ili kukabiliana na tatizo hilo imeweka utaratibu na sasa TAMISEMI itaenda kuzindua mfumo wa kielektroniki ambapo maombi ya uhamisho yatapitishwa kwa njia ya kielektroniki.

Alisema hatua hiyo itawezesha kuhakikisha watumishi katika maeneo ya vijijini wanabaki na kutoa huduma kwa wananchi.



Baadhi ya wabunge wakiingia Bungeni jijini Dodoma juzi, kuhudhuria vikao vya bajeti vinavyoendelea. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wenye teknolojia wasakwa kuwekeza General Tyre

BUNGE limeelezwa kuwa sasa serikali kupitia Shirika la Taifa la Maendeleo (NDC) inaendelea kutafuta mwekezaji mwenye uwezo wa kuwekeza teknolojia mpya katika kiwanda cha matairi mkoani Arusha.

Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, aliyasema hayo jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Arusha Mjini (CCM), Mrisho Gambo, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara.

Katika swali lake, Mbunge Gambo alihoji serikali ina mpango gani wa kufufua viwanda vya General Tyre na Pharmaceutical Industries Ltd ili kuongeza ajira na upatikanaji wa dawa nchini. Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Bashe alisema uwekezaji huo unatakiwa uendane na uhitaji wa bidhaa za matairi zilizopo sokoni.

Alifafanua kuwa tayari utaratibu wa kutangaza zabuni umefanyika ili kumpata mbia wa kufufua Kiwanda cha Matairi Arusha.

Hata hivyo, alisema katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo na Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda na Mkakati wake, viwanda vya dawa ni moja ya viwanda vya kipaumbele ikizingatiwa kuwa kiasi kikubwa cha fedha kinachotumika kuagiza dawa kutoka nje ya nchi kwa mwaka, ajira zinazopotea pamoja na umuhimu wa kuzalisha dawa kwa ajili ya usalama wa wananchi wake.

"Hivyo, Wizara inaona kuna umuhimu mkubwa wa kuharakisha kufikiwa kwa uamuzi wa kesi inayoikabili kiwanda cha TPI na pia kwa kuzingatia kuwa serikali inamiliki hisa asilimia 30 katika Kiwanda hicho ili kuruhusu mara moja kuanza kwa uzalishaji wa dawa," alisema.

Pia alisema serikali inatambua umuhimu wa kuwa na viwanda mbalimbali nchini vikiwamo viwanda vya matairi na dawa ili kuchochea uchumi wa nchi kwa kuzalisha bidhaa na ajira. Awali, Bashe alifafanua Kiwanda cha Matairi kilichojulikana kama General Tyre Arusha (kwa sasa Kiwanda cha Matairi Arusha) ni moja ya kiwanda kikubwa cha matairi katika ukanda wa Afrika Mashariki ambapo uzalishaji katika kiwanda hicho ulisimama mwezi Agosti 2007 baada ya kukosa fedha za kujiendesha husasan fedha za kununua malighafi.

"Wizara imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kukifufua kiwanda hicho ili kufikia malengo ya Serikali ya kujitosheleza kwa mahitaji ya matairi nchini, kuokoa fedha nyingi za kigeni zinazotumika kuagiza matairi kutoka nje na kuzalisha ajira," alisema.

Alibainisha Wizara iliunda timu ya wataalam ili kufanya tathmini juu ya njia bora ya kuendesha kiwanda hicho.

"Matokeo ya utafiti huo yalionesha kuwa mitambo na teknolojia iliyopo imepitwa na wakati na hivyo ikashauriwa kuwa mashine na mitambo ya kisasa ifungwe ili kuleta tija na ufanisi katika uzalishaji,"alisema.

# HOTUBA YA WAZIRI WA MAJI MHESHIMIWA JUMAA HAMIDU AWESO (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA MAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

**Siku ya Alhamisi tarehe 6 Mei, 2021, Waziri wa Maji, Mheshimiwa Jumaa Hamidu Aweso (Mb), amewasilisha Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maji kwa Mwaka 2020/2021. Hotuba hii ina maeneo makuu manne, ambayo ni hali ya sekta ya maji nchini; utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2020/2021; malengo na mpango wa kuboresha huduma ya maji kwa Mwaka 2021/2022; na maombi ya fedha kwa Mwaka 2021/2022. Hapa chini ni muhtasari wa hotuba hiyo. Hotuba kamili inapatikana katika tovuti ya wizara www.maji.go.tz.**

## 1. HALI YA SEKTA YA MAJI NCHINI

### 1.1. Hali ya Rasilimali za Maji

Tafiti zilizofanywa na Wizara mwaka 2019 zimeonesha kuwa rasilimali za maji zinazoweza kupatikana kwa mwaka kwa matumizi mbalimbali nchini ni wastani wa mita za ujazo **bilioni 126.** Kati ya hizo, mita za ujazo bilioni 105 ni maji juu ya ardhi na mita za ujazo **bilioni 21** ni maji chini ya ardhi. Kwa kuzingatia makadirio ya idadi ya watu **milioni 55.9** katika mwaka 2019, kiasi cha maji kilichopo kwa kila mtu kwa mwaka ni takribani wastani wa mita za **ujazo 2,250.** Kiasi hicho ni juu ya wastani wa mita za ujazo 1,700 ambacho ni kiwango cha chini cha mahitaji ya maji kwa mtu kwa mwaka kinachokubalika kimataifa.

### 1.2. Hali ya Huduma za Ubora wa Maji

Hali ya ubora wa maji katika vyanzo vya maji kwa maeneo mengi nchini inaonesha kuimarika. Hiki ni kiashiria kwamba afya ya ikolojia katika vyanzo hivi inaendelea kuimarika na maji yake yanaweza kutumika baada ya kuchakatwa kulingana na matumizi yanayokusudiwa. Aidha, mifumo yetu ya usambazaji wa maji kwa ajili ya matumizi ya majumbani imeendelea kusambaza maji yanayokidhi viwango vya ubora wa maji vya kitaifa licha ya kuwepo kwa changamoto kwenye baadhi ya maeneo.

### 1.3. Hali ya Huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini na Mijini

Hadi kufikia Machi, 2021 hali ya upatikanaji wa huduma ya maji vijijini imefikia wastani wa **asilimia 72.3** kutoka wastani wa **asilimia 70.1** mwezi Machi, 2020. Kwa upande wa mijini hali ya upatikanaji wa huduma ya majisafi imeongezeka kutoka **asilimia 84** mwezi Machi, 2020 hadi asilimia 86 mwezi Machi, 2021.

## 2. UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA 2020/21

### 2.1. Hali ya Upatikanaji wa Fedha

Wizara ya Maji kwa mwaka 2020/21 iliidhinishiwa bajeti ya jumla ya **Shilingi bilioni Mia Saba Thelathini na Tatu nukta Mbili Nane Nne (TZS 733.284); kati ya fedha hizo Shilingi bilioni Ishirini na Nane nukta Mbili Saba Tano (TZS 28.275) zilikuwa ni fedha za Matumizi ya Kawaida na Shilingi bilioni Mia Saba na Tano nukta Zero Zero Tisa (TZS 705.009)** zilikuwa ni fedha za maendeleo. Hadi mwezi Aprili 2021, Wizara imepokea jumla ya **Shilingi bilioni Mia Tatu Tisini na Sita nukta saba saba moja (TZS 396.771)** sawa na asilimia 54.1 ya bajeti yote. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni Mia Tatu Sabini na Sita nukta Nane Mbili Mbili (TZS 376.822)** ni fedha za maendeleo sawa na asilimia 53.4 ya bajeti ya maendeleo. Kwa upande wa fedha za Matumizi ya Kawaida, kiasi kilichopatikana ni **Shilingi bilioni Ishirini nukta Tatu Nne Tisa (TZS 20.349) sawa na asilimia 72.**

### 2.2 Miradi na Programu mbalimbali zilizotekelezwa katika mwaka 2020/21

Wizara ya Maji imeendelea kutekeleza miradi na programu mbalimbali za maji nchini kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji inayolenga kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025. Hali ya utekelezaji wa miradi na programu hizo katika mwaka 2020/21 ni kama ifuatavyo:-

### 2.3 Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji

Rasilimali za maji nchini zinasimamiwa na kuendelezwa kupitia Bodi za Maji za Mabonde tisa ambazo zimepewa majukumu ya kufanya tathmini na ufuatiliaji wa rasilimali hizo; kuhifadhi na kuthibiti uchafuzi wa vyanzo vya maji; kugawa maji kwa sekta mbalimbali kwa kuzingatia mahitaji na kiasi cha maji kilichopo; na kuendeleza rasilimali za maji. Katika kutekeleza majukumu hayo, Wizara imejenga na kukarabati vituo 159 vya kufuatilia mwenendo wa rasilimali za maji; imeweka mipaka katika vyanzo vya maji 25; imetoa vibali vya matumizi ya maji 1,096; na imesanifu kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa mawili na malambo sita ya maji.

### 2.4 Huduma za Ubora wa Maji

Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kuhakiki na kufuatilia ubora na usalama katika vyanzo vya maji na mitandao ya kusambaza maji kwa lengo la kulinda afya ya jamii na ikolojia. Katika mwaka 2020/21, Wizara iliendelea kuhakiki ubora wa maji nchini katika vyanzo kwa ajili ya matumizi ya majumbani, viwandani, umwagiliaji, ujenzi na utafiti pamoja na ubora wa majitaka yanayorudishwa kwenye mazingira. Vilevile, Wizara iliendelea na utekelezaji wa Mkakati wa Uondoaji wa Madini ya Fluoride kwenye maji ya kunywa na kupikia katika mikoa iliyoathirika zaidi na madini hayo (fluoride belt); kufuatilia ubora wa madawa ya kutibu na kusafisha maji; na kuimarisha maabara za maji ili ziweze kufanya kazi kwa ufanisi.

### 2.5 Huduma za Usambazaji Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini

Serikali kupitia Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) katika mwaka 2020/21 ilipanga kutekeleza jumla ya miradi **1,169.** Hadi kufikia mwezi Machi 2021, miradi **355** yenye vituo 6,687 vya kuchotea maji imekamilika na inahudumia wananchi **1,984,575.** Aidha, utekelezaji wa miradi 814 unaendelea na upo katika hatua mbalimbali.

### 2.6 Utekelezaji wa Miradi yenye Changamoto za Muda Mrefu

Serikali imekuwa ikifanya maboresho ya kimuundo na kisheria katika kuhakikisha huduma ya majisafi na usafi wa mazingira inakuwa bora na endelevu. Pamoja na maboresho yanayofanyika, bado hali ya utoaji wa huduma ya maji na usafi wa mazingira siyo ya kuridhisha hususan vijijini na katika Miji Mikuu ya Wilaya na Miji Midogo ambako kumekuwa na changamoto za usimamizi na uendeshaji wa miradi ya maji. Hali hiyo kwa kiasi kikubwa ilichangiwa na mfumo uliokuwepo ambapo usimamizi na utekelezaji wa shughuli za sekta

# TANGAZO

ya maji ulikuwa kwenye wizara mbili tofauti ambazo ni Wizara ya Maji na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI). Hali hiyo ilisababisha mlolongo mrefu katika kuchukua hatua kunapotokea ukiukwaji wa taratibu za kiutumishi au kiutendaji. Kufuatia changamoto hizo za kimfumo, tarehe 10/05/2018 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alifanya maamuzi ya kisera na kuelekeza kuhamishwa kwa majukumu ya utoaji wa huduma za maji kutoka OR-TAMISEMI kwenda Wizara ya Maji.

Kufuatia maamuzi hayo, Serikali ilianzisha Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) unaohusika katika ujenzi wa miradi na usimamizi wa huduma ya maji vijijini. Kuanzishwa kwa Wakala huo kumeenda sambamba na kurithi miradi yote ya maji ikiwemo ya vijiji 10 iliyokuwa inatekelezwa chini ya Halmashauri za Wilaya. Baadhi ya miradi ya maji iliyorithiwa imekuwa na changamoto ya kutokukamilika kwa wakati na mingine kukamilika bila kutoa maji. Jumla ya miradi 177 ilibainika kuwa na changamoto hizo ambapo hadi kufikia mwezi Machi 2021, jumla ya miradi 85 imepatiwa ufumbuzi na tayari imeanza kutoa huduma ya maji. Miongoni mwa miradi hiyo ni pamoja na miradi ya maji ya Ntomoko – Dodoma, Nyamtukuza – Geita, Mibono – Tabora, Rugeye – Mwanza, Malinyi – Morogoro, Muze group – Rukwa, Kinesi – Mara na Imalabupina-Ichwankima – Geita. Ukwamuaji wa Miradi hiyo unaendelea kwa kutumia Timu Maalum za Wataalam na tumezipa jina maarufu kama **" Water Rescue Teams".**

**2.7 Huduma za Usambazaji wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Mijini**

Serikali imeendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya maji inayolenga kuboresha upatikanaji wa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira mijini. Hadi mwezi Machi 2021, miradi 177 ya maji imeendelea kutekelezwa katika Miji Mikuu ya Mikoa, Miji Mikuu ya Wilaya, Miji midogo na Miradi ya Kitaifa ambapo miradi 67 imekamilika kwa gharama ya shilingi bilioni 759.211 na utekelezaji wa miradi 110 upo katika hatua mbalimbali. Baadhi ya miradi hiyo ni pamoja na:-

**(i). Mradi wa Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Jiji la Arusha**

Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) inatekeleza mradi wa ujenzi wa miundombinu ya usambazaji majisafi na uboreshaji wa huduma ya uondoshaji wa majitaka katika Jiji la Arusha unaogharimu takribani **Shilingi bilioni 520.** Hadi mwezi Machi 2021, utekelezaji wa mradi umefikia wastani wa **asilimia 62** na unatarajiwa kukamilika mwezi Oktoba 2021. Kukamilika kwa mradi huo kutaongeza uzalishaji wa maji kutoka lita milioni 40 hadi lita milioni 200 kwa siku, muda wa upatikanaji wa huduma ya majisafi kutoka saa 12 za sasa hadi saa 24 kwa siku pamoja na kuongeza huduma ya uondoshaji wa majitaka kutoka asilimia 7.6 za sasa hadi asilimia 30.

**(ii). Miradi ya Kuboresha Huduma ya Maji katika Jiji la Dodoma**

Mahitaji ya maji katika Jiji la Dodoma kwa sasa yanakadiriwa kuwa zaidi ya **mita za ujazo 103,000** kwa siku ambapo uzalishaji wa sasa ni **mita za ujazo 66,600** kwa siku. Katika kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali inaendelea kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika Jiji la Dodoma kwa kutekeleza mradi wa kutoa maji katika visima vya Ihumwa kwenda tanki la Njedengwa unaogharimu **Shilingi bilioni 2.4** ambao utekelezaji wake umefikia wastani wa **asilimia 70;** na ujenzi wa tanki la maji lenye uwezo wa kuhifadhi lita milioni 2.5 katika eneo la Chamwino ambao umefikia wastani wa asilimia 90. Aidha, uchimbaji wa visima nane (8) na ukarabati wa visima vitatu (3) umekamilika.

Vilevile, Serikali imeanza kuchukua hatua za muda mrefu zinazolenga kuondoa adha ya upatikanaji wa huduma ya maji kwa kuanza maandalizi ya mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria kuleta Jijini Dodoma. Hadi mwezi Machi 2021, upembuzi wa awali umekamilika na taratibu za kumpata Mtaalam Mshauri atakayefanya upembuzi yakinifu (Feasibility Studies) na usanifu wa kina (Detailed Design) zinaendelea. Aidha, taarifa za awali zinaonesha kuwa maeneo yatakayonufaika na mradi huo ni pamoja na baadhi ya maeneo ya mikoa ya Singida na Dodoma.

**(iii) Mradi wa Maji Tabora, Igunga na Nzega**

Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya India kupitia Benki ya Exim-India imetekeleza mradi wa upanuzi wa mtandao wa maji kutoka Ziwa Victoria kwenda Miji ya Tabora, Igunga, Nzega na vijiji 102 vilivyopo kilometa 12 pembezoni mwa bomba kuu kwa gharama ya takriban Shilingi bilioni 617. Mradi huo una uwezo wa kuzalisha kiasi cha mita za ujazo 54,145 kwa siku na kuhudumia zaidi ya wakazi milioni 1.2 wa maeneo mbalimbali ya mradi. Ninapenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa mradi huo unatoa huduma kwa wanufaika na ulizinduliwa rasmi tarehe 30 Januari, 2021 na Hayati Daktari John Pombe Joseph Magufuli aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania .

**(iv) Mradi wa kutoa Maji Ziwa Victoria kwenda Miji ya Tinde na Shelui**

Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya India kupitia Benki ya Exim-India inatekeleza mradi wa kuboresha huduma ya maji katika miji ya Tinde na Shelui. Mradi huo unatekelezwa kwa gharama ya Shilingi bilioni 24.752. Usanifu wa mradi huo umekamilika na utiaji saini wa Mkataba wa ujenzi ulifanyika tarehe 25 Februari 2021. Utekelezaji wa mradi huo unatarajiwa kukamilika katika kipindi cha miezi 12 kwa kutumia fedha zilizobaki kutoka kwenye Mradi wa maji wa Tabora, Igunga na Nzega.

**(v) Mradi wa Maji wa Same – Mwanga – Korogwe**

Mradi wa maji wa Same – Mwanga – Korogwe unatekelezwa katika miji ya Same na Mwanga pamoja na vijiji 38 vilivyomo kandokando ya bomba kuu katika Wilaya za Same, Mwanga na Korogwe. Mradi huo unatekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na BADEA, OFID, SAUDI Fund na Kuwait Fund. Mradi utakapokamilika utazalisha maji lita milioni 103.7 kwa siku na utawanufaisha wananchi wapatao 438,930.

Tarehe 25 Desemba, 2020 Wizara ilisitisha mikataba kwa wakandarasi wanaotekeleza mradi huo baada ya kuonekana wakisuasua katika ukamilishaji wa mradi. Wizara imeamua kwamba sehemu ya utekelezaji wa mradi inayohusu miundombinu ya usambazaji itafanyika kwa utaratibu wa Force Account kutumia Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es salaam (DAWASA) ili kukamilisha kwa haraka kazi hizo. Aidha, kwa kazi nyingine taratibu za manunuzi ya kumpata mkandarasi akayekamilisha mradi zinaendelea. Mradi huo unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba 2021 na utaondoa kero ya maji ya muda mrefu kwa wananchi wa maeneo husika.

**(vi) Mradi wa Kuboresha Huduma ya Maji katika Miji 28**

Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya India inatekeleza mradi wa kuboresha huduma ya maji katika miji 28 ya Tanzania Bara na mji mmoja visiwani Zanzibar unaogharimu Dola za Marekani milioni 500. Hadi mwezi Machi 2021, taratibu za manunuzi kwa ajili ya kuwapata Wakandarasi wa ujenzi zimekamilika na wakandarasi watakuwa maeneo ya miradi mwezi Mei 2021.

**(vii) Miradi ya Maji katika Maziwa Makuu ya Victoria, Tanganyika na Nyasa**

Serikali imeanza kutekeleza miradi ya kutoa maji kwenye maziwa makuu ya Victoria, Tanganyika na Nyasa kupeleka kwenye vijiji vilivyomo kandokando mwa maziwa hayo. Hadi

mwezi Machi 2021, usanifu wa kina na uandaaji wa makabrasha ya zabuni ya miradi ya kutoa maji Ziwa Victoria na Ziwa Tanganyika umekamilika. Mradi wa Ziwa Victoria unatarajiwa kuhudumia wananchi 2,854,292 kwenye vijiji 300 na mradi wa Ziwa Tanganyika utahudumia wananchi 616,000 wa vijiji 73. Utekelezaji wa miradi hiyo unatarajiwa kuanza katika mwaka wa fedha 2021/22 kwenye baadhi ya vijiji. Kwa upande wa Ziwa Nyasa, usanifu wa kina wa mradi unaendelea na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2021.

**(viii) Miradi mingine inayotekelezwa**

Miradi mingine inayoendelea na utekelezaji ni pamoja na Mradi wa Kukabiliana na Athari za Mabadiliko ya Tabianchi katika Mkoa wa Simiyu; Miradi ya Kuboresha Huduma ya Majisafi katika Mkoa wa Dar es Salaam na baadhi ya Maeneo ya Mkoa wa Pwani ya Kibaha, Kisarawe, Mkuranga, Chalinze na Bagamoyo; Mradi wa Mugango - Kiabakari - Butiama; pamoja na Mradi wa kuboresha huduma ya majisafi katika Mji wa Orkesumet.

**3. MAFANIKIO YALIYOPATIKANA**

Katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021, mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa miradi mbalimbali katika Sekta ya Maji ni pamoja na: kuongezeka kwa kiwango cha upatikanaji wa huduma za maji nchini kutoka asilimia 70.1 vijijini na asilimia 84 mijini mwaka 2019/20 hadi asilimia 72.3 vijijini na **86** mijijni; kuzinduliwa kwa miradi mikubwa ya maji ya Tabora – Igunga - Nzega pamoja na Isaka – Kagongwa baada ya kazi kubwa ya utekelezaji wake kukamilika; kukamilika kwa utekelezaji wa miradi **422** ya maji ambapo kati ya hiyo ya vijijini ni miradi **355** na mijini miradi 67; kuanza kutoa huduma ya maji kwa miradi **85** iliyokuwa na changamoto baada ya kupata ufumbuzi; kuongezeka kwa kasi ya utekelezaji wa miradi ya maji na kupungua kwa gharama za ujenzi kutokana na kutumia utaratibu wa **force account** ambapo zaidi ya miradi **150** imetekelezwa; na kuongezeka kwa idadi za maabara za ubora wa maji zenye ithibati kutoka moja (1) ya Mwanza hadi kufikia Saba (7).

**CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA NA HATUA ZINAZOCHUKULIWA**

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana wakati wa utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2020/21 Wizara inakabiliwa na changamoto mbalimbali. Changamoto hizo ni pamoja na uharibifu wa vyanzo vya maji, upatikanaji mdogo wa fedha za kutekeleza miradi ya maji, utendaji usioridhisha wa wakandarasi na watendaji, mwamko mdogo wa wananchi kulipia huduma ya maji kwa imani kuwa maji ni ya bure kutoka kwa Mungu na miundombinu inatoka kwa Mzungu; na upungufu wa Wataalam wa Sekta ya Maji.

Wizara inaendelea kuchukua hatua kukabiliana na changamoto hizo ikiwa ni pamoja na kuchukua hatua kali kwa wakandarasi na watendaji wanaoshindwa kutekeleza majukumu yao, kuimarisha vyombo vya utoaji huduma na kutoa elimu kwa wananchi.

**4. MPANGO WA UTEKELEZAJI KWA MWAKA 2021/22.**

Mpango wa Utekezaji wa miradi ya maji kwa mwaka 2021/22 umeshirikisha wadau mbalimbali wakiwemo Waheshimiwa Wabunge katika kuibua miradi ya kipaumbele. Aidha, Wizara itaendelea kuimarisha ushirikiano na Ofisi ya Rais-TAMISEMI katika kuibua, kutekeleza na kusimamia miradi ya maji katika Halmashauri za Wilaya nchini. Utaratibu huu utawezesha kufikia malengo ya Sekta ya Maji kwa haraka na uhalisia. Mpango na Bajeti kwa mwaka 2021/22 umezingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Malengo ya Maendeleo Endelevu 2016 – 2030, Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji, Sera mbalimbali za Taifa, Mikakati, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (2020 – 2025) na Maagizo na ahadi alizozitoa Mheshimiwa Rais na Viongozi wengine wa Kitaifa; pamoja na maoni ya waheshimiwa Wabunge.

Katika mwaka 2021/22, Serikali imepanga kuendelea kuweka msisitizo katika usimamizi wa watendaji, uvunaji wa maji ya mvua hususan kwenye maeneo kame, usimamizi wa Vyombo vya Utoaji Huduma za Maji Vijijini (CBWOs), kutumia Chuo cha Maji kikamilifu na kuimarisha kitengo cha uchimbaji wa visima na ujenzi wa mabwawa. Aidha, mipango imejikita katika maeneo ya usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji; huduma za ubora wa maji; huduma za usambazaji maji na usafi wa mazingira vijijini na mijini; na utekelezaji wa kazi mbalimbali katika Taasisi zilizo chini ya Wizara na masuala mtambuka kama ifuatavyo:-

**4.1. Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za maji**

Wizara itaendelea kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji wa takwimu za hali ya rasilimali za maji; kusimamia utoaji wa vibali vya matumizi ya maji ili kupunguza migogoro; kuratibu uchimbaji wa visima vya maji nchini; kutangaza vyanzo **28** kuwa maeneo tengefu ya vyanzo vya maji; kubaini vyanzo vipya kwa lengo la kuvitunza; kudhibiti uchafuzi wa vyanzo vya maji katika maeneo mbalimbali; pamoja na kuimarisha ushirikiano na nchi wanachama katika usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za majishirikishi.

**4.2. Usimamizi wa Huduma ya Ubora wa Maji**

Wizara itaendelea kufuatilia ubora wa maji katika vyanzo na mifumo ya usambazaji kwa kukusanya na kuchunguza sampuli **15,000** za maji; kutoa elimu juu ya viwango vya ubora wa maji kwa ajili ya matumizi mbalimbali; kuhakiki ubora wa madawa ya kutibu maji; kutengeneza na kusambaza mitambo **800** ya kuondoa madini ya fluoride inayotumika ngazi ya kaya; kuimarisha uhakiki na kufuatilia ubora wa majitaka kwa kupima na kuhakiki sampuli **2,000** za majitaka; pamoja na kuendelea kuimarisha maabara za maji.

**4.3. Miradi ya Majisafi na usafi wa Mazingira**

Katika mwaka 2021/22, Serikali imepanga kutekeleza jumla ya miradi 1,527 ya maji katika maeneo ya vijijini na miradi 114 maeneo ya mijini ikiwemo miradi mipya, miradi ya upanuzi na ukarabati wa miundombinu. Vilevile, Serikali imepanga kuimarisha Taasisi zinazosimamia utoaji wa huduma za maji na usafi wa mazingira nchini vikiwemo vyombo vya watumia maji (CBWSOs), Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira, Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini na kusimamia ufuatilia wa utekelezaji wa miradi.

Serikali imepanga kutekeleza miradi ya maji kwa kutumia vyanzo vya maji vya maziwa makuu pamoja na mito mikubwa ya Rufiji, Ruvuma na Kiwira. Katika mwaka 2021/22, kwa upande wa mto Rufiji na mto Ruvuma, Serikali imepanga kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa miundombinu ya kupeleka maji katika miji iliyo karibu na mito hiyo. Aidha, Wizara itaanza ujenzi wa mradi kutoa maji mto Kiwira kupeleka katika jiji la Mbeya.

**5. MAOMBI YA FEDHA**

Wizara ya maji imeomba kuidhinishiwa na Bunge jumla ya shilingi 680,388,976,000 kwa ajili ya matumizi ya mwaka 2021/22. Kati ya fedha hizo, Matumizi ya Kawaida ni **Shilingi 33,758,976,000** ambapo **Shilingi 15,273,812,000** sawa na **asilimia 45.2** ni kwa ajili ya kugharamia Matumizi Mengineyo (OC) na Shilingi **18,485,164,000** sawa na **asilimia 54.8** ni kwa ajili ya kulipa mishahara (PE) ya watumishi wa Wizara na Chuo cha Maji. Jumla ya bajeti ya maendeleo ni **Shilingi 646,630,000,000** ambapo kati ya fedha hizo, Shilingi **346,630,000,000** sawa na **asilimia 53.6** ni fedha za ndani na Shilingi **300,000,000,000** sawa na asilimia 46.4 ni fedha za nje.





# Waziri aonya watakaoshindwa kutekeleza mkataba wa mteja

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WIZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, imesema haitasita kuwachukulia hatua za kinidhamu viongozi na watumishi watakaoshindwa kutekeleza majukumu yao kikamilifu kwa matakwa ya mkataba wa huduma kwa mteja.

Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omar Kipanga, alisema hayo jana jijini hapa alipokuwa akizindua mkataba wa wizara hiyo.

Aliagiza taasisi zote kuhakikisha zina mkataba wa huduma kwa mteja kulingana na mwongozo wa utekelezaji wa mkataba huo. "Niwaagize watumishi wote wa wizara, wakuu wa idara na vitengo, wakuu wa vyuo kufanya kazi kwa kuzingatia taaluma zao ili mkataba wa huduma kwa mteja utekelezwe kwa viwango vinavyotarajiwa.

"Mhakikishe mna mikataba iliyo hai na mnatekeleza kwa viwango vinavyotakiwa na zile zilizo na mikataba iliyopitwa na wakati, ihuwishwe ili kuendana na wakati," alisema.

"Mkataba utatumika kama njia ya mawasiliano na wateja wetu na sisi wizara tutahakikisha tunatoa huduma bora na za kuridhisha,"alisema.

Aliwaasa viongozi wateuliwa kuwasimamia watumishi ili kutoa huduma bora kwa wateja na kwamba wizara itawapongeza viongozi na watumishi watakaofanya vizuri huku akiwasisitiza kuzingatia sheria, miongozo na kanuni wakati wa utekelezaji wa mkataba huo.

"Ufanisi katika utekelezaji wa mkataba huu hautaletwa na viongozi na watumishi wa wizara pekee bali utategemea ushirikiano wa wadau wote wa wizara, hivyo niwaombe wadau wote kutoa ushirikiano thabiti ili kuhudumiwa kwa ubora na viwango tulivyoahidi," alisema.

Naye Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Leonard Akwilapo, alisema utekelezaji wa mkataba huo utafungua ukurasa mpya wa uwajibikaji kwenye maeneo ya kazi.

Alisema pia mkataba huo utawapa mbinu mbalimbali za kuwahudumia wateja na kuwataka kufanya kazi kwa ufanisi.

"Kuna mambo mengi tumetoa ahadi bungeni na tutakuwa na mjadala mkubwa kwa ajili ya mstakabali wa elimu yetu, tujipange kwa hili pia," alisema.

Naye, Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu wa Wizara hiyo, Moshi Kabengwe, alisema ili kuhakikisha mkataba unafanya kazi kwa ufanisi, wizara imeandaa fomu maalum ambayo itaonyesha mrejesho wa huduma alizopata mteja kama ameridhika au la.

Alisema wizara imechapisha vitabu 6,000 vya mkataba huo ambavyo vitasambazwa kwenye taasisi zote za wizara hiyo.



Mamalishe akiandaa chakula kwa ajili ya kuwauzia wateja wake ili kujikimu kimaisha katika Mtaa wa Swaswa, jijini Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Kalemani ahimiza umuhimu wa miradi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, amewataka watumishi wa wizara hiyo kuweka kipaumbele katika utekelezaji wa miradi ya kimkakati ili ikamilike kwa wakati na kuisaidia jamii katika shughuli za kiuchumi.

Dk. Kalemani alisema hayo jijini Dodoma, wakati wa ufunguzi wa baraza maalum la wafanyakazi wa wizara hiyo.

Alisema kila mfanyakazi anapaswa kuona ana wajibu wa kufanya kazi kwa bidii, ubunifu, kujituma na kuacha kufanya kazi kwa mazoea ili kuwezesha miradi ya kimkakati ikamilike kama ilivyopangwa.

Dk. Kalemani alitaja miradi hiyo kuwa ni pamoja na ujenzi wa Bwawa la Kufua Umeme wa Maji la Julius Nyerere (JNHPP).

Alisema bwawa hilo linatarajiwa kuzalisha megawati 2,115 ambazo zikijumlishwa na megawati 1,500 zinazozalishwa na vyanzo mbalimbali hivi sasa zitaifanya Tanzania kuwa na umeme utakaotosheleza mahitaji yake na ziada kuuzwa kwa majirani.

Lengo la kuanzisha mradi huo, alisema ni moja ya juhudi za serikali za kupunguza gharama za umeme kwa wananchi kwa sababu uzalishaji wake ni wa gharama nafuu kulinganisha na vyanzo vingine.

Mradi mwingine ni wa gesi asilia iliyosindikwa (LNG) ujenzi wa mradi wa bomba la mafuta ghafi wa jumla ya Kilometa 1,443 kutoka magharibi mwa Uganda mpaka katika bandari ya bahari ya Hindi, Tanga.

Dk. Kalemani alisema mradi wa Treni ya mwendo kasi (SGR) ya kutumia umeme ni miongoni mwa miradi ya kimkakati na wa kwanza kujengwa Afrika Mashariki na awamu ya kwanza imekamilika.

Alisema njia ya reli kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro umbali wa kilimita 160, imekamilika na kutoka Morogoro hadi Singida utajengwa kwa awamu.

"Huu ni mradi mkubwa sana kwetu na Kenya wanataka na wao kuanza kujenga," alisema.

Aidha, alisema katika usambazaji umeme vijijini bado kuna changamoto kutokana na wananchi kutokuwa na ari ya kutaka kuunganishiwa umeme.

Alitaka elimu kuendelea kutolewa kwa wananchi ili wafahamu manufaa ya kutumia umeme.

"Nimekwenda kuwasha umeme kwenye kijiji kimoja katika Wilaya ya Kongwa umeme umepitishwa kiliomita 12 lakini wananchi walioomba kuunganishiwa umeme ni saba tu," alisema Dk. Kalemani.

Mwakilishi wa Kamishna wa Kazi kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera Bunge, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Tulia Msemwa, alisema mabaraza ya wafanyakazi ni muhimu kwa kuwa yana majukumu mbalimbali ikiwamo kutoa ushauri na maoni.

"Baraza lina uwezo wa kutathimini shughuli za wizara, linatoa ushauri baada ya kutathimini utekelezaji wa malengo ya kiutendaji" alisema.

# Majaliwa kubariki Wiki ya Ubunifu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, leo anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika Wiki ya Mashindaano ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (MAKISATU) yanatarajia kufanyika katika Uwanja wa Jamhuri, jijini hapa.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mkurugenzi wa Capital Space, Abdalla Mbwana, alisema lengo la wiki hiyo ni kuonyesha maendeleo ya wabunifu pamoja na ubunifu wao.

Mbwana alisema mashindano hayo ya ubunifu yana lengo pia la kuibua vipaji vya wabunifu mbalimbali ambao wamejitokeza kushiriki katika mashindano hayo.

Alifafanua kuwa maonyesho hayo yamedhaminiwa na kampuni ya simu za mkononi ya Vodacom pamoja na CRDB, Ifakara Innovation, NMB, Tigo, Ubalozi wa

Uholanzi, UNCDF na UN WOMEN.

Alisema kaulimbiu ya wiki ya ubunifu ni 'Ubunifu kwa Uchumi wa Kidigitali Stahimilifu na Jumuishi' ikiwa na msisitizo wa kuelekeza wabunifu kujituma ili kuinua uchumi wa taifa.

Hata hivyo, alisema wiki ya ubunifu ni pamoja na kuonyesha maendeleo kwa njia za ubunifu ambazo zinatatua kero mbalimbali zinazojitokeza.

Alisema kwa sasa maonyesho hayo yametimiza miaka mitano na uzinduzi utafanyika jijini Dodoma huku kilele kikiwa jijini Dar es Salaam Mei 22, mwaka huu.

Mbwana alisema maonyesho hayo ya ubunifu yametawanywa katika mikoa mbalimbali ikiwamo Mbeya, Morogoro, Iringa, Zanzibar na Tanga.



## Wanawake wapiga hatua ujenzi nyumba

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

ASILIMIA 60 ya wanawake mkoani Mbeya, wamefanikiwa kujenga nyumba zao wenyewe, kutokana na juhudi walinazo katika kufanya kazi kwa bidii.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na wakazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, ambapo alisema asilimia 60 ya wanawake mkoani humo, wanaendesha maisha yao bila kutegemea msaada wa mwanamume na kwamba wamefanikiwa kumiliki nyumba zao.

Alisema ukiangalia nyumba zilizojengwa na wanawake ambao kwa kiasi kikubwa ni wajasirimali zinavutia kwa sababu zimezingatia ubora na kiwango kinachotakiwa kwa kuzingatia ramani ya mipango miji inayotolewa na serikali.

Chalamila aliwapongeza wanawake hao kwa kuachana na mambo yasiyofaa na kuamua kuwekeza kwenye ujenzi wa nyumba ambayo ni hazina isiyoharibika na itarithiwa na vizazi.

Wanawake wa Mbeya ni miongoni mwa wanawake Tanzania ambao wanajituma sana katika kutafuta riziki, wanajishughulisha na mambo mbalimbali ili kujiongezea kipato ukilinganisha na wanaume ambao asilimia kubwa wanapenda kulelewa, ukionyeshwa nyumba inayomilikiwa na mwanamke utashangaa kwa sababu ya uzuri wake, hakika tuige mfano wao," alisema Chalamila.

Aliongeza kuwa kulingana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia pamoja na ukuaji wa miji, wananchi wanapaswa kujenga nyumba za kisasa ambazo zinavutia miji kuliko ilivyo sasa ambapo katikati ya Jiji la Mbeya zimejengwa nyumba za hovyo.

Aliwataka maofisa mipango miji kuendelea kutoa elimu kwa wananchi wanaonunua ardhi kuhakikisha wanafuata ramani zinazotolewa kujenga nyumba za kisasa badala ya kujiamulia kutumia michoro yao.

Baadhi ya wanawake walisema kuwa siri ya kumiliki nyumba nzuri na za kisasa ni kufanya kazi kwa bidii na kubana matumizi ya fedha inayopatikana.

Mmoja wa wanawake, Salome Anangisye, mkazi wa Isyesye jijini Mbeya, alisema baadhi yao wanapenda vitu vya anasa wanasahau kuwa binadamu anatakiwa kula, kuvaa na kuishi mahali pazuri pa kuvutia.

Alisema miongoni mwa faida za kumiliki nyumba ni kuondokana na msongo wa mawazo kutokana na madeni ya kodi kwenye nyumba za kupanga, lakini kupata amani ya moyo na hewa safi.

# Mwenyekiti wa CCM afunguka madai ya DED kumtishia maisha

**Na Grace Mwakalinga,** MBOZI

MWENYEKITI wa Chama cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Songwe, Heneriko Mkola, amekanusha madai yaliyotolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi, Hanji Godigodi, kuwa alimtishia maisha mbele ya Mkuu wa Mkoa huo, Nicodemas Mwangela, kutokana na kugoma kulipa madeni deni lake la zabuni Sh. milioni 18.

Akizungumza na Nipashe, Msola alisema kauli hiyo hakuwahi kuitoa popote, isipokuwa Mkurugenzi huyo aliamua kumchafua kwa maslahi yake binafsi.

"Kwa muda mrefu sasa nimekuwa nikiidai Halmashauri ya Mbozi, kiasi cha Sh.milioni 18 fedha za zabuni kutokana na huduma niliyokuwa naitoa, kutokana na Mkurugenzi kugoma kulipa deni hilo akitaka nilete nyaraka... tulifikishana hadi kwa Mkuu wa Mkoa wa Songwe Brigedia Generali, Nicodemas Mwangela ili kupata suluhu ya deni hilo," alisema Msola.

Alisema uamuzi wa kwenda kwa Mkuu wa Mkoa, Mwangela, ulilenga kukaa meza moja ili kujadili namna gani anaweza kulipwa deni hilo, kwani nyaraka zote mauzo anazo isipokuwa Mkurugenzi ndiye aligoma kulipa.

Baada ya kumalizika kwa kikao hicho kati ya Mkurugenzi, Mkuu wa Mkoa, Mwenyekiti wa CCM na wajumbe wengine wa Kamati ya Ulinzi na Usalama siku chache baadaye Mkurugenzi alidai majambazi walivamia nyumba ya jirani ambayo walidhani yake wakitaka kumuua.

Alisema baada ya tukio hilo Mkurugenzi huyo alienda kituo cha Polisi kutoa taarifa ambapo aliandika maelezo, na kwamba tukio hilo alilihusisha na kigogo ambaye alidai ni Mwenyekiti wa CCM.

Alisema polisi waliahidi kufanya upelelezi kubaini ni kina nani walihusika kufanya kitendo hicho, ambacho hakuna madhara yeyote yaliotokeo, na kwamba baada ya kukamilisha watatoa taarifa.

Mkola alieleza kusikitishwa na kauli hiyo kuwa imelenga kumchafua, kwa sababu yeye ni mfanyabiashara wa muda mrefu wilayani hapo na amekuwa akitoa huduma katika Ofisi za Halmashauri ya Mbozi kwa muda mrefu.

Alisema katika maisha yake yote ambayo kama mfanyabiashara amewahi kukopesha fedha zaidi ya milioni 200 na wakati mwingine baadhi ya watu hawalipi kabisa madeni hajawahi kutamka kauli ya kumtishia mtu, na kwamba Mkurugenzi huyo anayedai kutishiwa maisha mbele ya Mkuu wa Mkoa, Mwangela ambaye ndiye Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi angeweza kuchukua hatua mara moja.

Aliongeza kuwa suala la madai kwa Halmashauri ni la taasisi sio mtu mmoja, hivyo anaamini haki yake itapatikana kwa sababu anazo nyaraka zote za mauzo.

Alieleza kuwa licha ya maneno mengi kuzungumzwa hivi sasa yakimhusisha na yeye kuwa aliwashawishi madiwani kuazimia kutofanya kazi na Mkurugenzi hiyo hayana ukweli wowote, na kwamba uamuzi wa madiwani unatokana na upungufu walioyaona kiongozi huyo ikiwamo dharau kwa madiwani, wafanyakazi wenzake pamoja na matumizi mabaya ya fedha za miradi ikiwamo kahawa Sh. milioni 187.

"Mimi nimeishi Mbozi ni miaka 40 sasa sijawahi kukumbwa na kashfa kama hii licha ya kuwa ni mfanyabiashara ambaye natii kanuni na sheria zote za kibiashara, siku zote ukweli huchelewa kudhihirika, lakini naamini utajulikana na Mungu yupo atajibu," alisema Mkola.

Hivi karibuni Baraza la Madiwani wa Halmshauri ya Wilaya ya Mbozi, liliazimia kutofanya kazi tena Mkurugenzi, Hanji Godigodi kwa madai ya matumizi mabaya ya madaraka, ikiwamo ubadhirifu wa fedha za miradi na kutoa lugha za dharau kwa watumishi wenzake na madiwani.

Hata hivyo, Godigodi alikanusha madai hayo na kwamba ataendelea na kazi zake kama Mkurugenzi kwani alinyimwa nafasi ya kujieleza mbele ya baraza.



Meneja Mkuu wa Kampuni ya uendelezaji wa Jotoardhi Tanzania (TGDC), Mhandisi Kato Kabaka, akitoa mafunzo ya nishati ya jotoardhi kwa waandishi wa habari 27 kutoka mikoa ya Mbeya na Songwe, jana. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Mchakato kuvuna jotoardhi waiva

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

SERIKALI kupitia Kampuni ya uendelezaji wa Jotoardhi (TGDC), imeanza mchakato wa kununua mtambo wa kuchoronga visima vya kuvuna jotoardhi.

Lengo ni kuanza uzalishaji wa umeme na kuanzisha miradi ya maendeleo inayotokana na nishati hiyo.

Kauli hiyo ilitolewa na Meneja Mkuu wa TGDC, Mhandisi Kato Kabaka, wakati wa mafunzo yanayotolewa kwa wandishi wa habari kutoka Mikoa ya Mbeya, Songwe kuhusu uendelezaji wa jotoardhi nchini.

"Majukumu ya TGDC ni kuhimiza maendeleo ya rasilimali za jotoardhi nchini, kufanya tathmini ya rasilimali za jotoardhi kuanzia utafiti hadi hatua ya uendelezaji wake katika matumizi, kusimamia maeneo ya jotoardhi kwa ajili upatikanaji wa uhakika wa mtiririko wa mvuke kwenye mitambo ya uzalishaji wa umeme," alisema Mhandisi Kabaka.

Alisema lengo la kuanzisha mchakato huo ni kukabiliana na tatizo la upungufu wa uzalishaji wa umeme wa kutosha kutokana na sababu mbalimbali, hivyo serikali iliamua kuwa na vyanzo mbalimbali vya uzalishaji wa umeme vya nishati jadidifu vikiwamo jua, upepo na jotoardhi.

Mkurugenzi wa Maendeleo ya Biashara wa TGDC, Mhandisi Shakiru Kajugus, alieleza kuwa matumizi ya jotoardhi hutumika pia kuzalisha umeme kwa kutumia teknolojia mbalimbali ambapo nishati ya jotoardhi ( mvuke) ikiwa nyuzi joto 107 hasi nyuzi joto 300.

Alisema matumizi ya moja kwa moja ya nishati ya jotoardhi ni pamoja na kupasha moto mitambo viwandani, kupasha joto vitalu kwa ajili ya kilimo, kupoza na kugandisha, kukausha mazao ya kilimo, hutumika kama tiba pamoja na shughuli za kilimo.

Akifungua mafunzo hayo, Katibu Tawala wa Mkoa wa Mbeya, Mariam Mtunguja, alisema mafunzo hayo yatasaidia kukuza uelewa na umuhimu wa jotoardhi kwa wananchi.

Alisema kupitia wanahabari jamii itatumia vyema nishati zitokanazo na jotoardhi kwenye maeneo yote ya miradi ikiwamo kukuza uchumi na kufungua fursa mbalimbali za ajira.





# Wataka akaunti ya pamoja ya Muungano

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAJUMBE wa Baraza la Wawakilishi wametaka kuanzishwe kwa akaunti ya pamoja kati ya Serikali ya Muungano na ya Zanzibar ili kuhifadhi mapato yanayopatikana na kila upande wa Muungano kunufaika.

Waliyasema hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati wakichangia hutuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa mwaka wa fedha 2021/22.

Mwakilishi wa Malindi, Mohamed Ahmada, alisema suala la kuwapo kwa akaunti ya pamoja ya fedha limetajwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini utekelezaji wake haujafanyika hadi sasa.

"Suala la kuwapo kwa Tume ya Pamoja ya Usimamizi wa Fedha na mgawo wa asilimia 4.5 ambao Zanzibar inatakiwa kupata katika akaunti ya pamoja haujatekelezwa hadi sasa," alisema.

Mwakilishi wa Chaani, Nadil Abdullatif, alitaka utaratibu wa uwiano wa ajira za Serikali ya Jamuhuri ya Muungano ufuatwe ili kuimarisha Muungano huo.

Alimwomba Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais anayeshughulikia Muungano na Mazingira, Suleiman Jaffo, kupata nafasi ya kuhudhuria vikao vya Baraza la Wawakilishi kusikiliza baadhi ya wizara ambazo utendaji wake unahusisha moja kwa moja mambo ya Muungano.

Mwakilishi huyo alisema serikali zote mbili zimekuwa zikifanya juhudi za kuzipatia ufumbuzi kero za Muungano lakini utekelezaji wake unashindwa kufikiwa kutokana na baadhi ya watendaji kutotimiza majukumu yao na maagizo ya serikali.

"Tayari serikali zote mbili zimekubaliana suala la mgawanyo wa ajira za Muungano kupitia taasisi zake. Zanzibar itapata mgawo wa asilimia 21 wakati Jamhuri ya Muungano asilimia 39 lakini utekelezaji wake haujafanyika hadi sasa," alisema.

Naye Mwakilishi wa Shauri Moyo, Hamza Hassan Juma, alisema uteuzi wa mabalozi wa nje ya nchi hauleti ladha ya Muungano huku akidai Zanzibar imetengwa katika uteuzi huo.

Hamza ambaye ni Mnadhimu wa Baraza la Wawakilishi kutoka CCM, alisema ziko baadhi ya taasisi za Muungano lakini hazina sura halisi ya mgawanyo wa ajira kutoka pande mbili akitaja mojawapo kuwa ni Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

"Ukitembelea ofisi nyingi za ubalozi wa Tanzania zilizoko nje ya nchi ziko ambazo hazina hata Mzanzibari mmoja hata katika nafasi ya usafi wa ofisi.

"Tumepitisha makubaliano ya mgawanyo wa ajira katika taasisi za Muungano ambapo Zanzibar inastahiki kupata mgawo wa asilimia 21, lakini sijui kama utekelezaji wake kweli unafuatwa," alisema.




Spika wa Baraza la Wawakilishi, Zubeir Ali Maulid (wa pili kushoto waliokaa), akishiriki katika Iftar iliyoandaliwa kwa Wateja wa Benki ya Equity Zanzibar juzi. Wengine ni Mkuu wa Mikopo wa Benki ya Equity, Ramadhan Chakinja (wa pili kulia), Mkuu wa Masoko, Godwin Semunyu (kulia) na Meneja wa Tawi la Benki hiyo Zanzibar, Mbuka Sure. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Vitambulisho Mzanzibari Mkaazi vyaibua hoja nzito

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

BAADHI ya wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wametaka Idara ya Vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi kuongeza kasi ya kuwapatia wananchi vitambulisho hivyo ambavyo ni muhimu kwa ajili ya shughuli za kijamii ikiwamo masuala ya miamala ya fedha na uchumi.

Mwakilishi wa Pandani, Prof. Omar Fakih Hamad, wakati akichangia makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa mwaka 2021/22 jana, alisema upatikanaji wa vitambulisho hivyo ni kero kubwa na kikwazo kwa wananchi kupata huduma mbalimbali.

Alisema vitambulisho hivyo hivi sasa vinatumika kwa ajili ya kukamilisha mambo mbalimbali ya msingi ikiwamo upatikanaji wa mikopo ya elimu ya juu kwa wanafunzi na miamala ya fedha.

Prof. Omar alisema binafsi hana kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi jambo lililosababisha kutopiga kura katika uchaguzi mdogo wa Jimbo la Pandani.

"Mheshimiwa Spika, vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi ni muhimu. Si kwamba vinatumika kwa ajili ya shughuli za uchaguzi tu lakini hata za kijamii na kiuchumi katika masuala la kufanya miamala ya fedha," alisema.

Naye Mwakilishi wa Kojani, Hassan Hamad Omar, aliitaka Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC) kufanya maboresho ya uchaguzi na sheria zake ili kuhakikisha uchaguzi ujao unatoa ufumbuzi wa kero mbalimbali.

Alisema suala la vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi limesababisha wananchi wengi kushindwa kutumia haki ya kidemokrasia kupiga kura katika uchaguzi mkuu wa mwaka jana.

# SMZ kutoa bei elekezi mafuta ya kula

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Biashara na Viwanda, Omar Said Shaaban, amesema tayari wizara hiyo imeshafanya mchakato wa kutoa bei elekezi ya mafuta ya kula ambayo yamepanda bei na kusababisha usumbufu kwa wananchi.

Aliyasema hayo katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali kuhusu kupanda kwa bei ya bidhaa hasa mafuta ya kula.

Omar alisema tayari serikali imeshatangaza bei elekezi ya baadhi ya bidhaa zikiwamo sukari na unga wa ngano, hivyo muda si mrefu itatoa pia kwa mafuta ya kula.

Aidha, akijibu swali la Mwakilishi wa Micheweni, Shamata Shaame Khamis, aliyetaka kujua sababu za tofauti wa bidhaa kati ya Unguja na Pemba, waziri huyo alisema bei hutofautiana kutokana na gharama za usafirishaji.

Alisema wafanyabiashara wengi hushusha bidhaa zao katika Bandari ya Malindi Unguja na kuzisafirisha kwenda Pemba, hivyo gharama za usafiri husababisha wakati mwingine bei za bidhaa kwa Unguja kuwa ndogo kuliko Pemba.

Waziri alisema serikali ya Zanzibar imechukua jukumu la kupunguza kodi ya kutokutumia viwango vya kodi vya Jumuiya ya Afrika Mashariki ambayo kimsingi vingeongezeka bei za bidhaa muhimu za chakula hasa unga wa ngano, mchele na sukari kwa lengo la kuwapatia nafuu wananchi.

Alisema moja ya mipango ya serikali ni kujenga bandari ya kisasa Pemba ambayo kukamilika kwake kutaondoa kero hiyo.

Akichangia hotuba ya makadirio ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Mwakilishi wa Mtambwe, Habib Ali Muhammed, aliitaka serikali ijikite katika kupunguza bei za bidhaa ili kuwapunguzia gharama za maisha wananchi wa Zanzibar.

Alisema hivi sasa mafuta ya kula yenye ujazo wa lita tano yanauzwa Sh. 32,000 wakati yalikuwa yakiuzwa Sh. 17,000.

"Mafuta ya kula hasa kipindi hiki cha Ramadhani yanatumika kwa wingi lakini kutokana na bei kuwa juu, wananchi wanashindwa kupika maandazi na kalimati," alisema Mwakilishi wa Ziwani, Suleiman Makame Ali.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA
Katika mahakama ya Mwanzo ya Wilaya DODOMA MJINI.
Kituo cha DODOMA MJINI Mkoa DODOMA.
Usimamizi wa mirathi Na 122/2021.
KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU CHIKU HAMIS POCHELA WA DODOMA
KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA 122/2021
TANGAZO

(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)
Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na Mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 13 mwezi 05 mwaka 2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.

**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo tarehe 03 mwezi 05 mwaka 2021.

---

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA MOSHI.**
**WILAYA YA MOSHI**
**MAOMBI MADOGO NA. 306/2020**
**COURAGE WORLDWIDE IN (CWW).....................MLETA MAOMBI**
**DHIDI YA**
**1 . SECAO BUILDERS CO. LTD**
**2. THE BOARD OF THE RT OF MKOMBOZI CENTER FOR STREET CHILDREN**
**}WAJIBU MAOMBI**
**3. INDEPENDENT AGENCIES & COURT BROKERS LTD**

**KUITWA SHAURINI**
**KWA: THE BOARD OF THE REGISTERED TRUSTEES OF MKOMBOZI CENTER FOR STREET CHILDREN, POPOTE ULIPO**

Kwa kuwa mleta maombi ameleta madai ya kesi na yameelezwa katika nakala ya madai ambayo inapatikana katika Baraza la Ardhi na Nyumba Moshi. Shauri limepangwa kusikilizwa 12/05/2021 saa mbili na nusu (2:30) asubuhi mbele ya Mheshimiwa Mwenyekiti J.W.SILLAS, hivyo mnatakiwa kufika mahakamani wewe au mawakili wako .
ANGALIA : Kama hutahudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu Mahakama itasikiliza shauri hili na kutoa uamuzi upande mmoja .
Imetolewa na kutiwa saini na muhuri wa Baraza hili leo tarehe 29 mwezi April , 2021.

**MWENYEKITI**

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA

---

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya mwanzo MJINI MOROGORO**
**Usimamizi wa mirathi NO.140/2021**

Ombi la FILBET TEONAS ABDALLAH Kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu ANISET TEONAS ABDALLAH
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo tarehe 25/05/2021 kabla huyo mwambaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa.

Tarehe06/05/2021

---

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA MOSHI.**
**WILAYA YA MOSHI**
**MAOMBI MADOGO NA.279/2019**
**MICHAEL. P. MAKYAO......................................... MLETA MAOMBI**
**DHIDI YA**
**LILIAELI SHEDRACK SAMU**
**AGNESS P. MTENDE**
**JOSEPHINE ELINOHAKI MBOMBO**
**}WAJIBU MAOMBI**
**ELIBARIKI AMOS KILEO**

**KUITWA SHAURINI**
**KWA: LILIAELI SHEDRACK SAMU, POPOTE ULIPO**

Kwa kuwa mleta maombi ameleta madai ya kesi na yameelezwa katika nakala ya madai ambayo inapatikana katika Baraza la Ardhi na Nyumba Moshi. Shauri limepangwa kusikilizwa 25/05/2021 saa mbili na nusu (2:30) asubuhi mbele ya Mheshimiwa Mwenyekiti J.W.SILAS, hivyo mnatakiwa kufika mahakamani wewe au mawakili wako .

**ANGALIA :** Kama hutahudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu Mahakama itasikiliza shauri hili na kutoa uamuzi upande mmoja .
Imetolewa na kutiwa saini na muhuri wa Baraza hili leo tarehe 04 mwezi Mei , 2021.

**MWENYEKITI**

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA

---

**STRABAG INTERNATIONAL (T) BRANCH**

Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T.302 BGQ aina ya TOYOTA HILUX PICKUP, yenye Chassis no, JTFDE62440118654 ,Injini no, 3L5408535. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo karibu yake.

Taarifa ya Polisi.
BKE/TR/RB/1193/2020.

---

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI**
**IDAYA YA UHAMIAJI**

Telegramu: UHAMIAJI
Simu : 027-2751557
027-2752284
E- mail:riokilimanjaro@immigration.go.tz
Kumb. Na. IMM/MS/DN/UR/16305
MHARIRI,
GAZETI LA NIPASHE

OFISI YA UHAMIAJI MKOA,
S.L.P 1049
MOSHI
KILIMANJARO
Tarehe : 27/04/2021



**BWA ROBERT MULLU SABWAMI**

**HII NI TAARIFA KUWA:**

**BWA ROBERT MULLU SABWAMI NI RAIA WA KENYA**
Ambaye picha yake imeonyeshwa hapo juu,anaomba uraia wa Tanzania kwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya nchi .Yeye ni raia wa KENYA na Nchi atokayo ni KENYA.
Kazi yake /Shughuli zake ni Mwekezaji,
Anuani ya mwajiri wake /Shughuli zake ni 7640 MOSHI
Ameishi nchini tangu mwaka 2011, Pia amewahi kuishi Mkoa ..................................................................
,Mtu yeyeto mwenye sababu za kupinga mwombaji asipewe uraia, atume taarifa yake ya maandishi iliyosainiwa kwa:

Kamishna Jenerali wa Uhamiaji,
S.L.P 512
DARE ES SALAAM

**AIIS: FULAFU M.SHOMVI**
**KNY: AFISA UHAMIAJI MKOA, KILIMANJARO**

---

**KUPOTEA KWA CHETI**

BONIFACE B. MAGAYANE anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha sita chenye index namba S0132-0806 kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2010 katika shule ya Milambo High School mwaka 2010. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochocte cha Polisi. Polisi Taarifa: KIG/KIG/R-B/233032/2021.

---

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**ANNA NOAH LUKUMAY** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA RAUM** yenye namba za usajili **T 537 CRR** chasis namba **NCZ200064485** engine namba **INB457274,**yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa **CONTROL NAMBA 9910823468850**

---

**KUPOTELEWA NA KADI YA GARI**

**ELIAS EPHATHA KOKA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA TOYOTA CORONA YENYE NAMBA ZA USAJILI **T983 BHT, CHASIS: NO AT140-0009833,** ENGINE NO: **3AA-5113372.** YEYOTE ATAKAYE IONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **MAN/BAB/RB/231877/2021.**

---

**VYETI VIMEPOTEA**



**Elizabeth Raphael Ng'wandu** anatangaza kupotelewa na vyeti cha kidato cha sita chenye index namba **S2499-0930** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa Mwaka 2016 katika shule ya Sekondari Tusiime Secondary School. Na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1599-0023** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa Mwaka 2013 katika shule ya sekondari Baobao Secondary School.
Yeyote atakayeviona atoe taarifa kwenye kituo cha polisi kilicho karibu.
Taarifa ya polisi: **IRI/IRI/RB/233470/2021.**

---

**IN THE DISRICT LAND AND HOUSING TRIBUNAL FOR MARA AT MUSOMA**

**MISC. APPLICATION NO 403 OF 2020**

**EMMANUEL MAREGES WEREMA.................... APPLICANT**

**VERSUS**

1. **JOHN OUKO**
2. **THOBIAS DINDA......................................RESPONDENTS**

**SUMMONS/NOTICE**

**TO,**
**JOHN OUKO**
**THIBIAS DINDA**

The above mentioned applicant has instituted a suit in this Tribunal, against you, particulars of which are mentioned in a copy of the application which is obtainable from the registry of this tribunal .
**YOU ARE HEREBY SUMMONED TO APPEAR IN THIS TRIBUNAL**
In person [S] or by recognized agent(s) for mention on 07th may, 2021 at 08:00 am in the fore noon.

**TAKE NOTICE THAT**
In default of your appearance on the said day, the above mentioned suit shall be mentioned in your absence.

Given under my hand and seal of this Tribunal this ......29th....... day of ...March......, 2021.

Kitungulu, E.
Chairman
The District Land and Housing Tribunal – Mara

---

**JAMHURi YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**FORM II**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

**Katika Mahakama ya mwanzo MAKOLE**
**Usimamizi wa mirathi NA. 49/2021**

**Ombi la LUCY FELUKA LUGENDO kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi Marehemu HELENA PETRO MATONYA**

**KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA NA MIRATHI HII POPOTE ALIPO**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnano tarehe 23/05/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 05/05/2021.

Tarehe 5/5/2021
Sahihi ya Hakimu

---

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**PROTAS MAURUS MGENI** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 488 DEW - MITSUBISHI CANTER.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI.
TAARIFA YA POLISI: **NJ/TR/RB/101//2021.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA**
**MAHALI DODOMA**
**MAOMBI NA. 163 YA 2019**
**BAINA YA**
**YOWEL MUSSA NYAU.....................MDAI**
**DHIDI YA**
**JACKSON SEMU NYAU....................MDAIWA**

**KWA: JACKSON SEMU NYAU**

**POPOTE ULIPO**
**YAH: KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya Maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili.
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili wewe binafsi, Wakili au Mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 26.05.2021 saa 3:00 asubuhi. Kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa kuleta utetezi wako kwa maandishi.
ANGALIZO: kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu, Baraza likidhibitisha kuwa umepokea hayi ya Wito, Baraza linaweza kutoa Hukumu dhidi yako.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na lakiri /Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 05 ya Mwezi wa Mei,2021.

---

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# ICC yamhukumu kiongozi LRA afungwa miaka 25

MAHAKAMA ya Kimataifa ya Uhalifu wa Jinai (ICC), imemhukumu kifungo cha miaka 25 kiongozi wa zamani wa waasi wa Lord's Resistance Army (LRA), Dominic Ongwen.

Ongwen, anayefahamika kama White Ant, alipatikana na zaidi ya makosa 60 ikiwa ni pamoja na uhalifu dhidi ya binadamu na uhalifu wa kivita.

Waendesha mashtaka walisema Ongwen amepewa adhabu ndogo kwa sababu alikuwa ametekwa na LRA akiwa mtoto mdogo.

Kundi hilo la waasi liliundwa zaidi ya miaka 30 iliyopita, ikiendesha shughuli zake nchini Uganda na mataifa jirani.

**Ogwen alishiriki katika matukio mbalimbali ya uhalifu wa kivita Mei mwaka 2004...**

Ogwen mzaliwa wa kijiji cha Choorum Wilaya ya Amuru Kaskazini mwa Uganda, alitekwa nyara na kundi la waasi wa Josephy Kony, akiwa mvulana mdogo, wakati akielekea shule ya msingi Abili Koro.

Hiyo ni kwa mujibu wa maelezo yake, akidai alitekwa nyara mwaka 1988 akiwa na umri wa miaka 14.

Ripoti sahihi zinasemekana alitekwa akiwa na umri wa miaka tisa au 10, kwa kuwa alibebwa hadi kwenye kambi ya LRA na alikuwa hawezi kutembea.

Mama yake Ogwen, alipofahamishwa habari za kutekwa nyara kwa mtoto wake, aliamuwa kuwafuata wafuasi hao na baadaye watu walimkuta mama huyo amefariki pamoja na mumewe.

Baada ya muda akiwa na umri wa miaka 18, Ogwen alipewa cheo cha Brigedia wa kundi la waasi wa LRA na kuongoza kikosi cha Sinia.

Ogwen alishiriki katika matukio mbalimbali ya uhalifu wa kivita Mei mwaka 2004, walishambulia kambi ya ndani ya Lukodi wilayani Gulu, Kaskazini mwa Uganda.

Pia alishambulia kambi nyingine za ndani, ikiwamo ya Pajule, Odeke na Abok na kushiriki mauaji mbalimbali ya wananchi wasiokuwa na hatia, ubakaji na unyanyasaji wa kingono. **BBC**




Viongozi wa kundi la nchi saba tajiri duniani (G7), wakihitimisha mkutano wao wa kwanza kukutana baada ya miaka miwili kupita. Canada, Ufaransa, Ujerumani, Italia, Japan, Uingereza na Marekani zilikutana kujadili masuala mbalimbali ikiwamo kuliwekea vikwazo vipya jeshi la Myanmar ambalo lililofanya mapinduzi. **PICHA: DW**

## Kagame azungumza na mtoto wa Idriss Déby

**Kigali,** RWANDA

RAIS Paul Kagame, amempokea Abdelkerim Déby Itno (pichani chini) na kuzungumza naye kwa mujibu wa taarifa ya ofisi ya rais Rwanda.

Abdelkerim ni mjumbe maalum na Mkuu wa Ofisi ya Rais wa Baraza la Jeshi la Mpito Chad.

Hakuna maelezo zaidi yaliyotolewa kuhusu mazungumzo hayo yaliyofanyika juzi.

Rais Kagame anajulikana kama mmoja ambao walikuwa na uhusiano mzuri na makubaliano juu ya masuala yanayohusu bara la Afrika na Rais wa zamani wa Chad, Idriss Déby.

Utawala wa kijeshi nchini Chad, sasa unatishiwa na shinikizo kutoka kwa jamii ya kimataifa na Jumuiya ya Afrika, kutaka wanajeshi warudishe madaraka kwa raia.

Baraza kuu la kijeshi linaloongoza Chad, pia liko kwenye vita na vikundi vya waasi, ikidaiwa kuwa rais wa zamani Idriss Deby, aliuawa kwa kupigwa risasi alipokuwa akipigana kwenye vita hivyo mwezi uliopita.

Rais Kagame alipokea ujumbe wa Chad akiwa pamoja na Waziri wa Mambo ya Nje, Vincent Biruta na Meja Jenerali Joseph Nzabamwita na mkuu wa idara ya ujasusi (NISS).

Kwenye mitandao ya kijamii, wengine walisema kuwa kuonekana kwa Abdelkerim Idriss Déby kama balozi wa kaka yake mkubwa Jenerali Mahamat Idriss Déby, ilikuwa ishara kwamba familia ya Déby inaendelea kuimarisha utawala wake.

Kabla na baada ya kifo cha baba yao, kuliripotiwa malumbano kati wanawe kuhusu atakayemrithi.

Abdelkerim Idriss Déby, 29, alihitimu kutoka Chuo cha Jeshi cha Marekani (USMA) huko West Point mwaka 2015. Mwaka wa 2019 aliteuliwa kuwa Naibu Mkuu wa Ikulu ya Rais wa Chad.

Pia mwaka jana, aliongoza ujumbe wa Chad uliokutana na Waziri Mkuu wa Israeli, Benjamin Netanyahu kujadili kufungua ubalozi wa Chad, mjini Jerusalem. **BBC**



## Wanafunzi 30 waliotekwa waachiliwa huru

**Kaduna,** NIGERIA

WANAFUNZI 30 waliotekwa nyara Machi, mwaka huu na kundi la watu waliojihami kwa silaha za kivita Kaskazini mwa Nigeria, wameachiliwa.

Hatua hiyo ilikaribishwa Jumatano wiki hii na rais wa Nigeria, licha ya kukosolewa kwa kushindwa kuzuia mashambulio ya magenge ya wahalifu wanaofanya utekaji nyara wa watu wengi.

"Tunafurahi kuwa waliachiliwa. Tunawashukuru wahusika wote waliochangia kwa kitendo hiki cha kufurahisha," alisema Rais Muhammadu Buhari katika taarifa yake.

Jumla ya wanafunzi 39 walitekwa nyara Machi 11, katika chuo kikuu cha kaskazini magharibi mwa Nigeria, katika mji wa Kaduna.

Kundi la kwanza la wanafunzi 10, lilipatikana kwa msaada wa vikosi vya usalama katika wiki zilizofuatia shambulio hilo, huku wanafunzi 29 waliokuwa wamesalia walitekwa nyara kwa karibu miezi miwili.

"Makao makuu ya polisi yaliarifu serikali ya Jimbo la Kaduna, juu ya kuachiliwa kwa wanafunzi hao waliotekwa nyara Machi 11," Samuel Aruwan, Waziri wa Mambo ya Ndani wa Jimbo la Kaduna, alisema.

Visa vya utekaji nyara wa watu wengi shuleni vimeongezeka Kaskazini na katikati mwa Nigeria, vitendo vinavyotekelezwa na makundi ya wanamgambo wa Kiislamu au magenge ya wahalifu ambao huomba fidia au kuwa na uhusiano na makundi hayo yenye silaha. **RFI**

## Facebook bado yamzuia Trump kutumia mtandao

**Washington,** MAREKANI

BODI ya Usimamizi ya Facebook, imeshikilia uamuzi wake wa kupiga marufuku Rais wa zamani wa Marekani, Donald Trump kutuma maoni kwenye akaunti zake za Facebook na Instagram.

Hatua hiyo iliyowekwa baada ya kuchapisha maneno ya uchochezi, wakati mamia ya wafuasi wake walipovamia bunge la Marekani, Januari 6, mwaka huu.

Jopo hilo la kujitegemea, hata hivyo liliacha wazi uwezekano kwamba Trump anaweza kurudi kwenye tovuti yao maarufu, akisema haikuwa sawa kwa Facebook kuweka adhabu isiyojulikana na isiyo na kipimo ya kusimamishwa kwa muda usiojulikana.




# MBAPPE AKARIBIA KUSAINI MADRID

**PARIS,** Ufaransa

NYOTA wa Paris Saint-Germain, Kylian Mbappe anakaribia kujiunga na miamba wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, Real Madrid, kwa mujibu wa Diario AS.

Madrid imekuwa ikimwania Mbappe kwa muda mrefu na sasa wanaonekana kufikia pazuri kwenye makubaliano yao.

Mbappe mkataba wake kule Paris Saint-Germain unamalizika mwaka 2022 na hajaonyesha nia ya kutaka kusaini mkataba mpya.

Na sasa Madrid wameripotiwa kwamba wanakaribia kumsajili nyota huyo wa kimataifa wa Ufaransa.

Mbappe kwa muda mrefu amekuwa akiripotiwa kutaka kuondoka PSG na kwenda Madrid, ingawa mabingwa hao wa Ligue 1 bado wanajaribu kutaka kumsajili fowadi huyo mshindi wa Kombe la Dunia.




# 'Inter ina matatizo makubwa kifedha'

**MILAN,** Italia

MAKAMU wa Rais wa Inter Milan, Javier Zanetti, amesema mabingwa hao wa Serie A, "wana matatizo makubwa ya fedha" kuhusu kutojulikana kwa hatima ya umiliki wa klabu hiyo.

Sare ya Atalanta 1-1 dhidi ya Sassuolo wiki iliyopita ilimaanisha kwamba, Inter walitawazwa kuwa mabingwa wa Italia kwa mara ya kwanza tangu Jose Mourinho aliposhinda mataji matatu msimu wa 2009-10, na kumaliza umwamba wa Juventus wa kutwaa mara tisa mfululizo.

Licha ya kuwaongoza Inter kwenye mafanikio hayo, majaliwa ya Kocha Mkuu, Antonio Conte hayajulikani kutokana na hali ya mbaya ya kiuchumi iliyosababishwa na mlipuko wa virusi vya corona, huku wamiliki wa klabu hiyo, Suning Holdings Group wakifikiria kuiuza.

Ripoti kuhusu kuuzwa kwa klabu hiyo, zilikuja kwa mara ya kwanza katikati ya msimu huu na uvumi umesema wamiliki hao kutoka China ambao waliinunua mwaka 2016, wanapanga kuiuza kutokana na kuwa katika hali mbaya ya kiuchumi.

"Ni kweli kwamba, klabu ingeuzwa katikati ya msimu," amesema nahodha huyo wa zamani wa Inter Milan, Zanetti akiiambia La Nacion.

"Tulikuwa tunapitia kwenye hali ngumu sana ya kifedha, ingawa sio sisi pekee yetu ambao tupo kwenye hali ngumu.

Conte alitwaa taji lake la nne la Serie A msimu huu - na ni makocha watano tu walioweza kutwaa taji hili zaidi ya mara nne kwenye historia ya ligi hiyo.

# Nilijitoa sadaka kutua Chelsea – Tuchel

**LONDON,** England

THOMAS Tuchel amesema alijitoa sadaka kwa kuiacha familia yake na kuchukua nafasi ya kuinoa Chelsea na imekuwa na "thamani kila siku" baada ya kuweka historia ya kuwapeleka fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Blues hao walitinga fainali ya michuano hiyo kwa mara ya tatu kwenye historia yao baada ya kushinda 2-0 dhidi ya Real Madrid na kupata ushindi wa uwiano wa mabao 3-1 na kufuzu kwenye fainali itakayopigwa pale jijini Istanbul nchini Uturuki dhidi ya Manchester City, Mei 29, mwaka huu.

Kwa kufanya hivyo, Tuchel amekuwa kocha wa kwanza kwenye historia ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kufika fainali mara mbili mfululizo akiwa na timu tofauti.

Tuchel aliisaidia Paris Saint-Germain kutinga fainali ya michuano hiyo mwaka jana, na wakafungwa bao 1-0 na Bayern Munich.

Chelsea pia itacheza fainali ya Kombe la FA dhidi ya Leicester City Mei 15, mwaka huu na wanaongoza kwa pointi tatu wakiwa nafasi ya nne chini ya West Ham waliopo nafasi ya tano kwenye mbio za kumaliza kwenye nne bora ya Ligi Kuu England.

Tuchel amepoteza mechi mbili tu kati ya 24 (ushindi 16, sare 6), tangu achukue mikoba ya kuinoa timu hiyo Januari na amesisitiza sasa anajisikiwa yupo sehemu sahihi hapo Stamford Bridge.

"Imekuwa na ya thamani kila siku," alisema Tuchel kuhusu kujitoa sadaka alikofanya.

"Nilikuwa sehemu ya klabu ya aina yake tangu siku ya kwanza, nilipata sapoti kubwa tangu siku ya kwanza. Nina furaha kubwa kuwa katika sehemu ya timu hii."



# United yajipanga kumsajili Kane

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER United imejipanga kuinasa saini ya fowadi wa Tottenham Hotspur, Harry Kane, kwa mujibu wa BT Sport.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, United wana matumaini makubwa ya kupata saini ya nahodha huyo wa Timu ya Taifa ya England, ambaye majaliwa yake hayajulikani kule Spurs.

Kane mwenyewe alishaweka wazi kuwa ataamua hatima yake hapo Spurs mara baada ya michuano ya euro 2020, inayofanyika kuanzia Juni mwaka huu.

Dau ambalo limewekwa mezani ili kumpata kwa ajili ya kujiunga na United kwa Kane ni euro milioni 90.

Mpango huo ulikuwapo kwa muda mrefu ila huenda ukakamilishwa kwa haraka kutokana na presha ambayo wanaipata kutoka kwa mashabiki ambao waliandamana Jumapili ndani ya Uwanja wa Old Trafford jambo lililofanya mchezo wa United dhidi ya Liverpool upelekwe mbele.

Mashabiki wa United wamekuwa wakieleza kuwa hawana imani na Joel na Avram Glazer kutokana na uongozi wao kutokuwa na uwazi pamoja na kushindwa kupata mataji, jambo linalosababisha hasara kwao pamoja na suala la wao kujiunga na European Super League kwa kuwa imesababisha hasara kwao.






# MOUNT ADAI CHELSEA ILITAKIWA IFUNGE 5

**LONDON,** England

MASON Mount amesema kuwa ana furaha kubwa kuifungia Chelsea na kutinga kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya ambapo itakutana na Manchester City, lakini anahisi Real Madrid walitakiwa kufungwa zaidi ya mabao matano.

Chelsea inayonolewa na Thomas Tuchel iliibuka na ushindi wa mabao 2-0 juzi Jumatano kwenye nusu fainali ya pili pale Stamford Bridge, baada ya ile ya kwanza kutoka sare ya 1-1 na sasa imetinga fainali kwa uwiano wa 3-1.

Chelsea walikuwa kwenye kiwango bora zaidi usiku wa Jumatano na kujikuta wakiibuka na ushindi huo.

"Tulitakiwa kupata mabao matano," alisema Mount akiiambia BT Sport baada ya mchezo huo.

"Lakini jambo la muhimu ni kwamba tumeshinda. Tunataka kushinda kila mchezo.

"Tulikuwa na uwezo wa kupata mabao hadi matano, kwani baada ya 1-0 tulipata nafasi nyingi, lakini hatukuzitumia vizuri."

Kabla ya fainali hiyo, Chelsea itakutana na City Jumapili kwenye mchezo wa Ligi Kuu England.

# *Roma yatarajia makubwa kwa Mourinho*

**ROME,** Italia

JOSE Mourinho anaweza kufanya kazi kubwa na nzuri sana AS Roma, kwa mujibu wa kocha anayeondoka, Paulo Fonseca.

Roma ilitangaza Jumanne kwamba, Fonseca ataachia ngazi katika klabu hiyo mwishoni mwa msimu huu na nafasi yake itachukuliwa na Mourinho.

Raia huyo wa Ureno anarudi Italia baada ya kufukuzwa kule Tottenham Hotspur Aprili 19, mwaka huu baada ya miezi 17 ya kutoridhisha kule London.

Aliondoka Spurs akiwa wastani wa asilimia 51 ya ushindi kwenye mashindano yote.

Mourinho alishinda mataji matatu, Ligi, Coppa Italia na Ligi ya Mabingwa Ulaya wakati alipokuwa Kocha wa Inter Milan kati ya mwaka 2008 na 2010.

Na sasa Fonseca anatarajia kwamba, Mourinho atakuwa na mafanikio makubwa kwa timu hiyo yenye maskani yake makao makuu ya mji wa Italia.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# ZIDANE: CHELSEA ILISTAHILI KUTINGA FAINALI YA ULAYA

## Akiri wapinzani hao walikuwa bora zaidi katika mchezo huo huku akisema majeruhi...

**LONDON,** England

ZINEDINE Zidane amesema Chelsea ilistahili ushindi dhidi ya Real Madrid katika mchezo wa hatua ya nusu fainali ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na kutinga fainali.

**Madrid walifungwa 2-0 na Chelsea kwenye mchezo wa nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya juzi Jumatano, kwa mabao ya Timo Werner na Mason Mount pale katika dimba la Stamford Bridge.**

Ushindi huo umeifanya Chelsea kufuzu fainali kwa uwiano wa mabao 3-1 baada ya mchezo wa kwanza kutoka sare ya 1-1 na sasa itacheza na Manchester City kwenye fainali mwishoni mwa mwezi huu.

Los Blancos hao hawakuwa kwenye kiwango kizuri tofauti na walivyokuwa wakati wakishinda taji hilo la Ulaya mara tatu mfululizo chini ya Zidane kati ya mwaka 2016 na 2018.

Na Zidane amesisitiza wachezaji wake walipambana, lakini Chelsea walikuwa bora zaidi kwenye mchezo huo na sasa anaelekeza nguvu zake kwenye mbio za kuwania taji la Ligi Kuu Hispania, LaLiga, dhidi ya Barcelona na vinara Atletico Madrid.

"Tumezungumza mara nyingi msimu huu. Umekuwa mwaka mwenye majeruhi wengi, kupanda na kushuka na ndivyo tulivyokuwa," alisema Zidane akiwaambia waandishi wa habari baada ya mchezo huo.

"Licha ya yote, tulifanya vizuri kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya hadi tukafika hatua hii.

"Nafikiri tulistahili kufika hatua hii na tulibakia hatua moja kwenda fainali, lakini tunatakiwa kuwapa hongera Chelsea, ambao walikuwa bora sana usiku huu (juzi).

"Haibadilishi chochote. Najivunia kiwango cha wachezaj wangu walivyokionyesha na sasa ni wakati wa kumpumzika na kuangalia mechi nne za Ligi Kuu Hispania zilizobaki."

## ZISIKUPITE

### LIVERPOOL, KONATE SAFI

LIVERPOOL wamekubaliana kuhusu maslahi binafsi na nyota wa Ufaransa na RB Leipzig, Ibrahima Konate, 21, ambaye anajiandaa kujiunga na klabu hiyo ya Ligi Kuu England kwa mkataba wa miaka mitano. ***(Talk Sport)***

### TONEY AGEUKA LULU

KLABU ya West Ham imejiunga na Chelsea na klabu nyingine kwenye mbio za kuwania kumsajili, mshambuliaji wa Brentford, Ivan Toney, 25, ambaye dau lake la kumsajili ni pauni milioni 35. ***(Sun)***

### SALAH AJIPANGA KUONDOKA

NYOTA wa Misri, Mohamed Salah, 28, anataka kuondoka Liverpool na Paris St-Germain wanapanga kumpata mchezaji huyo kama Kylian Mbappe (22), ataondoka kipindi cha majira ya joto. ***(Le Parisien)***

### PSG YAMTAKA AURIER

PSG wanatafuta kuimarisha safu yao ya ulinzi na wamebainisha wanataka kumsajili beki wa Tottenham na Ivory Coast, Serge Aurier, 28. ***(RMC Sport in French)***

### WILLIAMS AWINDWA

KLABU ya Norwich City ipo kwenye mchuano na Southampton na West Ham katika mbio za kuwania kumsajili Brandon Williams, 20, kwa mkopo, kutoka Manchester United. ***(Sun)***

### CONTE ATAKIWA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur imefanya mazungumzo na kocha wa Inter Milan, Antonio Conte (51), kuhusu nafasi iliyo wazi ndani ya Spurs. Mazungumzo na Muitaliano huyo yamekuja baada ya Conte kuiwezesha Inter kutwaa taji lao la kwanza la Ligi Kuu baada ya miaka 11. ***(Corriere dello Sport,via Express)***

### MOURINHO KUMBEBA ROSSI

JOSE Mourinho anaweza kumtaka nahodha wa zamani, Daniele De Rossi, 37, kuungana naye kama kocha msaidizi baada ya kuteuliwa kuwa kocha mkuu wa AS Roma kwa msimu ujao. ***(Calciomercato)***

### LAMELA ANUKIA ROMA

KOCHA wa zamani wa Tottenham, Jose Mourinho atatazama uwezekano wa kumsajili kiungo wa kati wa Spurs, Erik Lamela, 29, na mshambuliaji wa Brazil, Lucas Moura (28). ***(Football.London)***

### HEE-CHAN ATAKIWA WEST

WEST HAM na Crystal Palace wanamfuatilia kwa karibu mshambuliaji wa RB Leipzig na Korea Kusini, Hwang Hee-chan, 25. ***(Telegraph)***

### TARAVES AINGIA SOKONI

BENFICA na RB Leipzig wanamfuatilia kwa karibu kiungo wa kati wa Leicester City, Sidnei Taraves, 19, lakini klabu yake ina mpango wa kumpatia mkataba mpya mchezaji huyo. ***(Football Insider)***

## KMKM kuikabili KVZ, ligi ikirejea

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

LIGI Kuu Zanzibar inatarajiwa kuendelea tena kuanzia mechi 22, mwaka huu, ambapo 'Maafande' wa KMKM watawakaribisha KVZ kwenye Uwanja wa Amaani wakati Polisi wataifuata JKU kwenye Uwanja wa Mau A Visiwani hapa.

Ligi hiyo itarejea tena kuanzia siku hiyo baada ya kusimama kwa muda wa mwezi mmoja ili kupisha ibada ya funga ya Ramadhani ambayo itamalizika wiki ijayo.

Ratiba iliyotolewa na Bodi ya Ligi Zanzibar (ZBL), inaonyesha msimu huu wa 2020/21 unatarajia kumalizika Juni 9, mwaka huu, ambapo bingwa mpya atajulikana pamoja na timu zitakazoshuka daraja.

Makamu Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Sheha Mohammed, alisema siku ya mwisho wa msimu kutakuwa na mechi mbili tofauti na hapo awali ilijulikana kutakuwa na michezo mitatu.

Sheha alisema kwa kushirikiana na ZFF katika kuelekea kumalizika michezo ya ligi, watakuwa wakali katika kuhakikisha vitendo vya upangaji wa matokeo vinaepukwa.

Aliongeza endapo hakutakuwa na vitendo vya upangaji wa matokeo na hujuma yoyote, bingwa halali atapatikana pamoja na timu itakayoshuka daraja.

## Muumin kuzindua albamu mpya Juni

**Na Sabato Kasika**

MWIMBAJI nyota wa muziki wa dansi na kiongozi wa bendi ya Special, Mwinjuma Muumin amesema amekamilisha albamu ya kwanza ya bendi hiyo na anajipanga kufanya utambulisho hivi karibuni.

Muumin aliliambia gazeti hili maandalizi ya albamu hiyo yalianza Januari, mwaka huu na malengo yake ni kuiweka hadharani ifikapo mwezi ujao.

Azitaja nyimbo zilizopo katika albamu hiyo ni pamoja na Yatima Mzee, Mwanangu, Fenesi na Kwa Mparange Sihami ambao amedai umepokelewa vizuri na mashabiki wa bendi hiyo kwenye mitandao ya kijamii.

"Yaani sasa ni kuangusha moja baada ya nyingine, tulianza na hizo nyimbo na tumepanga kufikia Juni tuwe tumekamilisha albamu ya kwanza ambayo tutaitambulisha kwa mashabiki wetu," alisema Muumin.

Aliongeza vionjo na mitindo mbalimbali ikiwamo nyimbo za mduara vilivyowekwa katika albamu hiyo vinasaidia kurudisha hadhi ya jina lake kwenye muziki wa dansi baada ya kupokelewa vyema na wadau waliozisikia kupitia mitandaoni.

# TFF YAFUNGUKA MAGOLI LIGI WANAWAKE HAYAJAFUTWA

**Na Adam Fungamwango**

SHIRIKISHO la Soka Tanzania (TFF), limetangaza kufuta matokeo ya mechi zote za timu ya ES Unyanyembe iliyocheza katika Ligi Kuu ya Wanawake, lakini ikibakisha mabao ya wachezaji ambayo nyota wake walifunga walipocheza dhidi ya timu hiyo.

**Mkurugenzi wa Mashindano wa TFF, Salum Madadi, alisema mabao ambayo yalifungwa wakati timu zinazoshiriki ligi hiyo walipokabiliana na ES Unyanyembe yataendelea kutambulika isipokuwa yale yaliyofungwa na wachezaji wa timu hiyo iliyoshushwa daraja.**

Madadi aliwataka wachezaji wa timu nyingine zilizobakia katika ligi hiyo kuendelea kujituma na kuongeza ushindani uliopo unasaidia kuwaimarisha na kuonyesha thamani waliyonayo nyota wote.

"Tunawataka wachezaji ambao wamefunga mabao kwenye mechi dhidi ya US Unyanyembe wasiwe na wasiwasi, waendelee kucheza, kujituma na kufunga mabao zaidi kwenye mechi nyingine ili kuleta ushindani na kuifanya Ligi Kuu ya Wanawake ambayo kwa sasa inaanza kuonyesha mwanga wa kutupiwa macho na mashabiki wa soka. Mabao ya wachezaji yote yako salama, kasoro wa US Unyanyembe tu. Kilichofutwa ni matokeo ya mechi tu ambayo timu hiyo imecheza," alisema Madadi.

ES Unyanyembe imeshushwa madaraja mawili baada ya kutotokea uwanjani Aprili 24, mwaka huu katika mechi dhidi ya Yanga Princess iliyotarajiwa kuchezwa kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

TFF imelazimika kutoa ufafanuzi kuhusiana na mbio za kusaka kiatu cha dhahabu baada ya kuwapo na sintofahamu iliyotokana na matokeo yote ya ES Unyanyembe kufutwa.

Kama mabao hayo yangefutwa, straika na nahodha wa Simba Queens, Oppah Clement ambaye alifunga mabao sita katika mechi dhidi ya timu hiyo hivyo angebakiwa na mabao 23 badala ya 29 aliyonayo sasa.

Oppah ndiye anayeongoza kwa ufungaji katika ligi hiyo akifuatiwa na Aisha Juma wa Alliance Girls mwenye mabao 23, na Aisha Masaka wa Yanga Princess mwenye idadi kama hiyo wakati Fatuma Mustapha wa JKT Queens akiwa na mabao 20 na mwenzake kwenye timu hiyo Stumai Abdallah akiwa na mabao 19.

Simba Queens ndio mabingwa watetezi na vinara wa ligi hiyo ambayo sasa inaelekea ukiongoni.



Wachezaji wa KMC FC wakifanya mazoezi kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam kwa ajili ya kuifuata Namungo katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa Jumapili mkoani Lindi. Kikosi hicho kitasafiri leo kuelekea mjini Ruangwa. **PICHA : JUMANNE JUMA**

# *Re-Focuss Africa kuibeba Zanzibar*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

WIZARA ya Habari, Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo imesaini mkataba wa miaka mitano na Taasisi ya Re-Focuss Africa kwa ajili ya kufanikisha maendeleo katika sekta zote zilizoko katika wizara hiyo, imefahamika.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Khamis Abdalla Said, alisema makubaliano yaliyofikiwa yana lengo la kuimarisha sekta za michezo, sanaa na utamaduni wa Zanzibar.

Kiongozi huyo alisema katika makubaliano yao mkataba huo umegusa katika mambo mawili kwa ujumla ikiwamo vijana, katika sekta ya michezo, utamaduni na sanaa.

Saidi alisema katika michezo mpango huo umejikita zaidi katika kuinua vipaji vya soka, mpira wa kikapu na riadha ambapo wanamichezo watapata fursa ya kupata mafunzo kupitia njia ya mtandao na baadaye watapokea vyeti ambavyo vitatambulika kimataifa.

"Hayo ndio makubaliano ambayo tumefikia katika kutekeleza malengo ya 2050, sisi wizara tunakiashiria chetu cha kupata medali nyingi za kimataifa kwa kufanya majaribio ya wachezaji wa ndani na wakimataifa kwenye mchezo wa riadha," alisema kiongozi huyo.

Aliongeza taasisi hiyo itashirikiana na kampuni nyingine mbalimbali, klabu maarufu pamoja na vyuo vikuu vinavyojihusisha kimichezo na sanaa ili Zanzibar ifaidike na udhamini huo.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa taasisi hiyo, Kanali Mstaafu Iddi Kipingu ameishukuru serikali kwa kuwakubali kushirikiana nao ili kufikia malengo ya kukuza vipaji vya vijana wa Zanzibar.

Kipindu alisema vijana ni muhimili mkubwa wa taifa na ndio wajenga nchi, kwa maana hiyo wanatakiwa kuendelezwa katika sekta mbalimbali.

# Michezo

Ijumaa Mei 7, 2021

Nipashe



Zidane: Chelsea ilistahili kutinga fainali

UKURASA 22




Kiungo mshambuliaji wa Yanga, Saido Ntibazonkiza (kushoto), akiwa katika mazoezi ya timu hiyo na golikipa, Metacha Mnacha kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Simba itakayochezwa kesho Jumamosi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

## Polisi yawaondoa hofu mashabiki

**Na Romana Mallya**

KAMANDA wa Kanda Maalum Dar es Salaam, Lazaro Mambosasa, amesema Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na vyombo vingine vimejipanga kuimarisha ulinzi na usalama katika mchezo wa watani wa jadi kati ya Simba na Yanga utakaochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam kesho.

Mechi hiyo ya marudiano ya Ligi Kuu Tanzania Bara itachezwa kuanzia saa 11 jioni huku mwamuzi wa kati akiwa ni Emmanuel Mwandembwa kutoka jijini Arusha.

Kamanda Mambosasa alisema Jeshi la Polisi limejipanga kuimarisha ulinzi kwa kuweka idadi kubwa ya askari katika maeneo yote na barabara zinazoingia na kutoka uwanjani hapo.

Kamanda huyo amewataka mashabiki na wapenzi wa soka kufika uwanjani mapema ili kuepusha msongamano wakati wa kuingia uwanjani hapo kwa sababu milango itafunguliwa mapema.

"Waepuke kuingia na chupa za maji majukwaani, kuingia na silaha ya aina yoyote, kupaki magari ndani ya uwanja pasipokuwa na kibali maalum na kukaa sehemu ambazo tiketi zao haziruhusu," alisema.

Pia amewataka mashabiki kushangilia mpira huyo kwa amani na utulivu lakini wakijiepusha na mihemuko na maneno ya uchonganishi baina yao.

# Simba, Yanga hakuna mnyonge

**Na Saada Akida**

## ●●● Kila upande wajiimarisha kutimiza malengo...

ZIKIWA zimebakia saa chache kuelekea pambano la watani wa jadi, uongozi wa Yanga umesema kikosi chao kipo imara kwa ajili ya kuondoka na pointi tatu muhimu katika mchezo huo wa marudiano wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaochezwa kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

**Hata hivyo Simba wenyewe wametamba wanahitaji kuukaribia ubingwa kupitia mchezo huo unaosubiriwa kwa hamu na mashabiki wa soka ndani na nje ya Tanzania.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Yanga, Nesreddine Nabi ambaye ameonyesha dhamira ya kufanya vizuri na kupata matokeo chanya kwenye mchezo huo dhidi ya Simba alisema vijana wake wako tayari na imara kwa ajili ya kuwavaa mabingwa hao watetezi.

Nabi alisema ana imani mchezo huo utakuwa na ushindani kwa sababu ya molari ya wachezaji wake ndani ya kikosi hicho ambao kila mmoja anatarajia kupambana ili kufikia malengo ya kuondoka na ushindi.

Kocha huyo alisema anaifahamu vyema Simba kwa sababu alifanikiwa kukutana nayo katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu huu akiwa anaifundisha Al Merriekh ya Sudan, hivyo ameisoma vizuri na hatarudia makosa kwenye mechi ya kesho.

"Naifahamu Simba kwa sababu nimefanikiwa kukutana nao nikiwa Sudan, ninaamini utakuwa mchezo wenye ushindani mkubwa kwa sababu kila mmoja wetu anahitaji kupata pointi muhimu ili kujiweka katika mazingira mazuri katika msimamo wa ligi," alisema Nabi.

Wakati huo huo Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli alisema kikosi chao kipo fiti na habari njema kwa mashabiki na wanachama wa timu hiyo ni kurejea uwanjani kwa kiungo wao wa kimataifa, Tuisila Kisinda ambaye alikuwa majeruhi.

Bumbuli alisema kuna uwezekano wa kumkosa kiungo wao Carlos Carlinhos ambaye yuko chini ya uangalizi wa madaktari ambayo wanaitazama afya yake kwa karibu.

"Nyota huyo (Carlinhos), anaweza kuukosa mchezo kwa sababu yuko katika uangalizi mkubwa wa madaktari, uwezekano wa kuwa naye katika kikosi cha timu hiyo kitakachocheza ni mdogo, lakini bado tunaendelea kusubiri taarifa ya mwisho kutoka kwa daktari," alisema Bumbuli.

Didier Gomes, Kocha Mkuu wa Simba alisema anaendelea kuwaimarisha wachezaji wake na anafanya hivyo kwa sababu anahitaji ushindi tu na si matokeo mengine.

Mfaransa huyo alisema anaamini kila mchezaji atatekeleza vizuri majukumu atakayopewa katika mechi hiyo inayotarajiwa kutoa taswira ya bingwa.

"Tunahitaji kupata matokeo mazuri, tumejipanga kuhakikisha tunacheza katika kiwango cha juu, tunawaheshimu wapinzani wetu kwa sababu nao wataingia uwanjani wakihitaji pointi tatu, itakuwa mechi ngumu lakini tutaonyesha ukubwa wetu," Gomes alisema.

Naye Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Haji Manara, alisema timu yake itaendelea kuvuna matokeo mazuri kwa sababu wanahitaji kuweka rekodi ya kuchukua ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara mara tano mfululizo.

Manara alisema kikosi chao kiko vizuri na wataingia uwanjani kucheza kwa tahadhari ili watimize malengo yao.

Alimtaja Feisali Salum 'Fei Toto', Saido Ntibazonzika kuwa ni moja ya wachezaji wazuri walioko katika kikosi cha wapinzani wao, lakini bado hawawapi nafasi ya kufanya vyema katika mchezo huo.

Simba yenye pointi 61, lakini imecheza mechi mbili pungufu inaongoza katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara ikifuatiwa na Yanga yenye pointi 57 wakati Mwadui FC ya Shinyanga inaburuza mkia.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >